BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

FEBRUARI, 2023

## YALIYOMO


**SEHEMU YA KWANZA** 4
1. UTANGULIZI 4
1.1 MUUNDO WA KAMATI 5
1.2 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI 6
1.3 HADIDU REJEA 7
**SEHEMU YA PILI** 8
2. **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MAFUNZO YA AMALI** 8
2.1 IDARA 8
2.2 MABARAZA NA BODI 8
2.3 PROGRAMU KUU 9
2.4 PROGRAMU KUU YA ELIMU YA JUU 10
A. CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA) 10
B. SKULI YA AFYA NA SAYANSI YA TIBA 15
C. SKULI YA KOMPYUTA, MAWASILIANO NA MAFUNZO YA HABARI ZANZIBAR (SCCM) 18
D. SKULI YA BIASHARA TAWI LA SUZA CHWAKA 21
2.5 PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI 23
2.6 PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU 30
2.7 PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI 40
3. **WIZARA YA AFYA** 44
3.1 IDARA 44
3.2 TAASISI 45
3.3 MABARAZA YA KITAALUMA/BODI 45
3.4 PROGRAMU KUU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA 46
3.5 PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA TIBA 52
3.6 PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI WA URATIBU WA WIZARA 60
4. **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** 65
4.1 PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII 66
KITENGO CHA PENCHENI JAMII 67
4.2 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA 70
A. WARATIBU WA SHEHIA YA MJINI MAGHARIBI 70

B. MASUALA YA UKATILI NA VITENDO VYA UDHALILISHAJI KWA WANAWAKE NA WATOTO ZANZIBAR ..... 73
4.3 PROGRAMU KUU YA UTAWALA UENDESHAJI WA WIZARA ..... 76
5. **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** ..... 80
5.1 SEKTA YA HABARI ..... 80
5.2 SEKTA YA VIJANA ..... 80
5.3 SEKTA YA UTAMADUNI ..... 81
5.4 SEKTA YA MICHEZO ..... 81
5.5 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI ..... 81
5.6 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ..... 93
5.7 PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA ..... 96
5.7.1 PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA TAFITI ..... 96
5.7.2 PROGRAMU NDOGO YA UENDESHAJI NA UTUMISHI ..... 99
**SEHEMU YA TATU** ..... 105
6. HITIMISHO ..... 105

## SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ni moja wapo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, (Toleo la 2020).

Kazi na majukumu ya Kamati hii yamebainishwa na kufafanuliwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

(a) kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
(b) kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
(c) kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi katika Wizara husika;
(d) kuchunguza na kufuatilia Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
(e) kuchambua Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka;
(f) kushughulikia Miswada ya Sheria inayokabidhiwa kwake na Spika;

(g) kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekeleaji wa ahadi hizo; na

(h) kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, katika Ripoti hii inajulikana kama "Kamati" ambapo ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Wizara nne (4) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Idara, Mashirika, Wakala, Mabaraza na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo. Wizara hizo ni hizi zifuatazo:

*(a)* Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali;
*(b)* Wizara ya Afya;
*(c)* Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na
*(d)* Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

## 1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati hii inaundwa na Wajumbe wafuatao:

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zawadi Amour Nassor | Mjumbe |

Aidha, Kamati hii inafanya kazi zake kwa kushirikiana na Makatibu na Msaidizi wa Mjumbe wafuatao:

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| **1.** | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| **2.** | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| **3.** | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

## 1.2 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa malengo yafuatayo:

(a) kufuatilia Maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2020/2021.
(b) kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2020/2021.
(c) kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka 2022/2023.
(d) kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara katika taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nane kama ifuatavyo:

(i) Tarehe 21/03/2022 hadi tarehe 25/03/2022 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 28/03/2022 hadi tarehe 01/04/2022 kwa upande wa Unguja.

(ii) Tarehe 09/08/2022 hadi tarehe 13/08/2022 kwa upande wa Unguja na kuanzia tarehe 16/08/2022 hadi tarehe 20/08/2022 kwa upande wa Pemba.

(iii) Tarehe 31/10/2022 hadi tarehe 04/11/2022 kwa upande wa Unguja na kuanzia tarehe 07/11/2022 hadi tarehe 11/11/2022 kwa upande wa Dar-es-Salaam.

(iv) Tarehe 23/01/2023 hadi tarehe 27/01/2023 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 30/01/2023 hadi tarehe 03/02/2023 kwa upande wa Unguja.

## 1.3 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2022/2023, Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo:

(a) Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la Mwaka 2020;

(b) Taarifa Rasmi za Baraza 'Hansard' za Baraza za Mwaka 2021/2022;

(c) Ripoti za Kamati kwa Mwaka 2021/2022;

(d) Hotuba za Bajeti za Taasisi za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2. WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MAFUNZO YA AMALI

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mafunzo ya Amali inaundwa na Idara Saba (7), Mabaraza Matatu (3), Bodi Tano (5) pamoja na Ofisi mbili (2) kama ifuatavyo:

### 2.1IDARA

(i) Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
(ii) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
(iii) Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;
(iv) Idara ya Elimu ya Sekondari;
(v) Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima;
(vi) Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu;
(vii) Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu; na
(viii) Ofisi Kuu Pemba.

### 2.2MABARAZA NA BODI

(i) Baraza la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia;
(ii) Baraza la Mitihani Zanzibar;
(iii) Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
(iv) Bodi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;
(v) Bodi ya Taasisi ya Elimu Zanzibar;
(vi) Bodi ya Huduma za Maktaba;
(vii) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na

(viii) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

## 2.3PROGRAMU KUU

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina Programu Kuu Sita (6) ambazo ni hizi zifuatazo:

(i) Programu Kuu ya Elimu ya Juu;
(ii) Programu ya Kuu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;
(iii) Programu Kuu ya Elimu ya Sekondari;
(iv) Programu Kuu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali;
(v) Programu Kuu ya Ubora wa Elimu; na
(vi) Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Programu hizi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinatekelezwa kwa mashirikiano makubwa ya utatu, yaani baina ya Serikali, wananchi, washirika tofauti wa maendeleo wa ndani na nje.

Pamoja na Programu hizo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pia kuna Miradi Mitano (5), ambayo ni hii ifuatayo:

(i) Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi;
(ii) Uimarishaji wa Elimu ya Msingi;
(iii) Uimarishaji wa Elimu ya Lazima;
(iv) Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali; na
(v) Uimarishaji wa Miundombinu katika Elimu.

## 2.4PROGRAMU KUU YA ELIMU YA JUU

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo moja ya Elimu ya Juu yenye madhumuni ya kutoa Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti itakayomuwezesha muhitimu kuweza kujiajiri au kuajiriwa. Sambamba na hilo, Elimu ya Juu jukumu la kusimamia utoaji wa Elimu Vyuoni na Kazini.

### A. CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ni Chuo Kikuu pekee cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Chuo kilianzishwa chini ya Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999 sambamba na marekebisho ya Sheria ya Chuo, Nam. 11 ya mwaka 2009. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar Nam. 7 ya mwaka 2016, ambapo Sheria hiyo ilifuta Sheria zilizoanzisha Chuo cha Uongozi wa Fedha - Chwaka (ZIFA), Chuo cha Taaluma za Afya - Mbweni na Taasisi ya Maendeleo ya Utalii - Maruhubi (ZIToD).

Vile vile, kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali iliridhia kuunganisha Taasisi ya Chuo cha Teknolojia ya Kilimo - Kizimbani (KATI) kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na kuwa Skuli ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Sambamba na hilo, katika mwaka huo huo wa fedha 2019/2020 Serikali pia ilianzisha Skuli Mpya ya Utibabu wa Meno ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo kimeanzisha Skuli Mpya ya Kompyuta, Mawasiliano na Taaluma za Habari, Skuli hii inatokana na kuunganishwa kilichokuwa Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar na

kuwa sehemu ya SUZA mwaka 2020, ambapo mabadiliko hayo yamapelekea ukuaji mkubwa wa Chuo.

Vile vile, Chuo hiki kinatekeleza shughuli zake kuu za msingi ambazo ni kufundisha, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaaluma. Chuo kina miaka 21 tangu kianzishwa kwake na kinafundisha programu 67 katika ngazi za Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Shahada ya Kwanza, Stashahada na Cheti.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)**

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(a) Matumizi ya Mfumo Mpya wa Manunuzi umeleta changamoto ya kucheleweshа kupatikana Wazabuni wa Miradi na Manunuzi ya Chuo.
(b) Mishahara midogo ya SUZA kulinganisha na vyuo au Taasisi nyengine, hii inapelekea wanataaluma wengi kuchukua likizo bila ya malipo kwa ajili kutafuta maslahi yaliyobora nje ya Chuo.
(c) Uhaba wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia yenye kukidhi uhitaji halisi uliopo kwa Kampasi zote za Chuo. Kozi za Sayansi Asilia, Kilimo pamoja na Afya zinauhitaji mkubwa wa vifaa vya maabara, kemikali pamoja na vitenganishi ambavyo vinahitaji gharama kubwa kuvinunua na kuvihifadhi. Chuo hulazimika baadhi ya muda kutumia maabara za nje ya Chuo kwa ajili ya kuendesha mafunzo kwa vitendo.
(d) Upungufu wa wahadhiri wa ngazi zote unaopelekea kutegemea zaidi walimu wa muda (part timers). Kwa sasa Chuo hulazimika kutumia

gharama kubwa ya mapato ya ndani kwa ajili ya malipo ya walimu wa muda. Pia Chuo kinakabiliwa na tatizo la wahadhiri wenye sifa wanaoendana na vigezo vya Chuo Kikuu. Suala hili linatokana na Chuo kurithi walimu ambao hawana vigezo vinavyotambulika na TCU;

(e) Uhitaji mkubwa wa ukarabati wa miundombinu kutokana na uchakavu wa majengo karibu kila Kampasi ya Chuo. Chuo kimerithi majengo mengi ambayo yamechakaa na yanahitaji gharama kubwa kuyatengeneza. Chuo kinaendelea kutenga fedha kidogo kidogo kwa ajili ya ukarabati ambao haukidhi haja ya mahitaji yaliopo.

(f) Uchache wa vifaa vya kufundishia kama vile kompyuta karibu kila kampasi ya Chuo. Studio ya Redio pamoja na Kituo cha Mafunzo ya Kidigitali navyo vinakabiliwa na upungufu wa vifaa.

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(a) Kamati inaishauri Serikali kuwapatia vibali vya ajira Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa ajili ya kuajiri wafanyakazi wapya ili kupunguza nakisi ya wafanyakazi wa muda ambao wanatumia fedha nyingi za Serikali.

(b) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaongezea bajeti ya mishahara Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili wafanyakazi waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuondokana na dhana ya kutafuta maslahi bora katika vyuo vya nje.

(c) Kamati pia inaishauri Serikali kuwatengea bajeti ya maendeleo kwa ajili ya kujenga miundombinu mipya pamoja na kufanya ukarabati mkubwa

wa majengo katika kampasi zake zote zinazosimamiwa na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

(d) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar kutenga bajeti maalum kwa ajili ya kukiendeleza Chuo Kikuu kwa upatikanaji wa vifaa vya kisasa katika maabara zetu kwa lengo la kutoa wahitimu waliobobea katika fani zinazohitajika kwa maendeleo endelevu ya Taifa hili.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA SAYANSI BENJAMIN WILLIAM MKAPA TAWI LA SUZA PEMBA**

(a) Ukosefu wa uzio katika eneo la Skuli ya Sayansi Benjamin William Mkapa, hali inayopelekea uvamizi wa maeneo ya Skuli kwa shughuli za kijamii ikiwemo wanyama kufungwa ndani ya eneo pamoja na wanajamii kupita katikati ya eneo la Skuli hiyo.

(b) Uhaba wa rasilimali watu pamoja na vitendeakazi katika Skuli ya Sayansi, hali inayosababisha kupungua ufanisi wa utendaji kazi katika Skuli hiyo.

(c) Ukosefu wa Kituo cha Afya katika mazingira ya Skuli, hali inayosababisha kuwapa wakati mgumu wanafunzi wa skuli hiyo pale wanapopata matatizo ya kiafya hasa wakati wa usiku.

(d) Ukomo wa matumizi ya fedha kwa Skuli hiyo baada ya kuunganishwa na SUZA, hali inayozorotesha utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Skuli na kutofikia malengo iliyojipangia kwa wakati.

(e) Uchakavu wa majengo ya Skuli ya Sayansi pamoja na ukosefu wa usafiri wa kudumu kwa walimu na wanafunzi wa Skuli hiyo hali inayosababisha walimu kuchelewa kuanza kwa vipindi vya masomo kwa wakati.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaushauri Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kujenga uzio katika Skuli ya Sayansi ya Benjamin William Mkapa Tawi la SUZA Pemba, kwa ajili ya kuwa na mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia.

(b) Kamati inapendekeza kwa Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kuajiri Wakufunzi wenye uwezo pamoja na sifa katika Skuli ya Sayansi Benjamin William Mkapa Tawi la SUZA Pemba, kwa ajili ya kuweza kusomesha wanafunzi wa kada mbali mbali ili kupunguza kuchukua walimu wa muda nje ya skuli.

(c) Kamati inaushauri Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kuipatia Skuli ya Sayansi ya Benjamin William Mkapa Tawi la SUZA Pemba vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia, ili waweze kwenda sambamba na kasi za mabadiliko ya elimu duniani.

(d) Kamati inaushauri Uongozi wa Skuli ya Sayansi ya Benjamin William Mkapa Tawi la SUZA Mchanga Mdogo Pemba kuwatumia wananchi au wanajamii wa Mchanga Mdogo katika suala la ulinzi wa skuli hiyo, kwani wao ndio wako karibu na mazingira hayo na pia wanajamii au wananchi wa eneo hilo.

(e) Kamati pia inapendekeza kwa Uongozi wa Skuli ya Sayansi ya Benjamin William Mkapa iliopo Pemba kuandaa pamoja na kuweka miongozo na taratibu za kufanya shughuli mbali mbali katika skuli hiyo kwa wanafunzi wa Cheti na Diploma ikiwemo masuala ya usafi wa mazingira pamoja na bustani badala ya kutegemea fedha za matumizi mengineyo Ofisi Kuu.

## B. SKULI YA AFYA NA SAYANSI YA TIBA

Skuli ya Afya na Sayansi ya Tiba imeanzishwa mwaka 2016 baada ya kuunganishwa na Skuli ya Tiba na Sayansi za Afya iliyokuwa chini ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) pamoja na Chuo cha Sayansi za Afya kilichokuwa chini ya Wizara ya Afya Zanzibar ambacho kilianzishwa kwa msaada wa Serikali ya Oman mwaka 1989.

Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba majukumu yake makuu ni kufundisha, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi wa shughuli za kiafya pamoja na kutoa huduma za taaluma ya afya kwa jamii.

### CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA AFYA NA SAYANSI ZA TIBA

(a) Uhaba wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia yenye kukidhi uhitaji halisi uliopo katika Kampasi ya Skuli. Wanafunzi wengi wemeendelea kukosa fursa ya kujiunga katika mafunzo ya kozi za afya kutokana na ufinyu wa madarasa.

(b) Upungufu wa wahadhiri wa kozi zote unaopelekea kutegemea zaidi walimu wa muda (part timers). Kwa kipindi cha robo ya pili (Oktoba - Disemba) Skuli imetumia jumla ya shilingi Milioni Mia Moja Hamsini na Nane, Laki Moja na Sitini na Nne, Mia Tatu na Thelathini na Nane (158,164,338,000/=) kwa kuwalipa walimu wa muda mfupi.

(c) Uchache wa ofisi kwa wafanyakazi na wakufunzi.

(d) Uhaba wa vifaa vya afya pamoja na kompyuta kwa lengo la kufundishia wanafunzi.

(e) Uhitaji mkubwa wa vifaa ikiwemo meza na viti kwa ajili ya wanafunzi na walimu.

(f) Mfumo wa manunuzi umekuwa ukichukuwa muda mrefu kwa kuwa Mfumo huu bado mpya na unachangamoto katika kutoa huduma na mara nyingi huwa haupatikani kwa urahisi.

(g) Mfumo wa Manunuzi umekuwa ukitumia sehemu kubwa ya bajeti kutokana na muundo wake wa kufanya kazi, ambapo vitu vya bei ya chini hupelekea kununuliwa kwa bei ya juu sana.

(h) Ukosefu wa uzio kwa baadhi ya maeneo ya Skuli unaopelekea baadhi ya wanyama waharibifu na watu wasiohusika kuingia kwenye eneo la skuli na kuhatarisha usalama wa wanaskuli na majengo.

(i) Uvamizi wa maeneo ya skuli kwa ajili ya shughuli za kijamii ikiwemo kilimo na maakazi.

(j) Uchakavu wa miundombinu ya maji safi na maji machafu katika dakhalia za wanafunzi unaopelekea ukosefu wa maji safi na kuhatarisha afya za wanafunzi na wanaskuli wengine wanaoishi katika mazingira ya hayo.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kufanya mazungumzo ya pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ili kulitafutia ufumbuzi tatizo la miundombinu ya maji safi na maji machafu lililochukua muda mrefu katika dakhalia za wanafunzi kwa ajili ya kuokoa afya za wanafunzi hao.

(b) Kamati inapendekeza kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kupitia Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba kuliangalia upya suala la uchukuaji wa walimu wa muda kutoka nje ya Skuli ili kupunguza matumizi makubwa ya fedha zilizokusudiwa kufanya maendeleo ya skuli na badala yake kutumika kwa kuwalipa walimu wa muda.

(c) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuharakisha ujenzi wa uzio wa Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba (Mbweni) ili kuwaepusha na ujenzi holela na uvamizi wa maeneo kwa ajili ya shughuli za kijamii ikiwemo kilimo na biashara.

(d) Kamati inaishauri Serikali katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya madarasa mapya pamoja na dakhalia katika Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba au kutafuta Mikopo na Wafadhili ili kuweza kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi wanaomba kujiunga na Skuli hiyo ambapo wengi wao wanakosa fursa za kujiunga kwa sababu ya uchache wa madarasa mfano halisi, mwaka 2022/2023. Idadi ya wanafunzi waliomba kujiunga na Skuli hiyo wakiwa na sifa ni 800 na waliopata nafasi ni wanafunzi wasiozidi 50, hali inayosababisha kutopatikana kwa wataalamu wa kutosha wa ndani pamoja na kuikosesha Serikali Mapato.

(e) Kamati inaipongeza Skuli kwa kufanya tafiti na maandiko mbali mbali na kutambulika Kimataifa kwenye Sekta ya Sayansi ya Afya.

(f) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Mamlaka ya Manunuzi iliopo chini ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kufanya kikao cha pamoja ili kutatua changamoto zinazozikabili Taasisi zote za Serikali juu ya suala zima la utumiaji sahihi wa

Mfumo Mpya wa Manunuzi (e-proz) hali inayowasababishia usumbufu mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yao pamoja na upotevu wa fedha za Serikali.

## C. SKULI YA KOMPYUTA, MAWASILIANO NA MAFUNZO YA HABARI ZANZIBAR (SCCM)

Skuli ya Kompyuta, Mawasiliano na Mafunzo ya Habari Zanzibar imeundwa mwaka 2020 tokea kuanzishwa kwake ina miaka miwili ambapo majukumu ya msingi ni kufundisha na kutoa huduma bora za kitaaluma kwa jamii ya watu wa Zanzibar pamoja na Tanzania Bara kwa ujumla.

Skuli hii kwa sasa inaratibu na kufundisha programu saba (7) ikiwemo:

(a) Programu za Shahada ya Uandishi wa Habari;
(b) Diploma ya Uandishi wa Habari na Cheti;
(c) Programu ya Uzamili ya Kompyuta ya Sayansi;
(d) Programu ya Shahada ya Kompyuta Sayansi;
(e) Programu ya TEHAMA;
(f) Programu ya Shahada ya TEHAMA na Uhasibu; na
(g) Programu ya Stashahada za Kompyuta ya Sayansi na TEHAMA.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA KOMPYUTA, MAWASILIANAO NA MAFUNZO HABARI ZANZIBAR**

(a) Uhaba wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia yenye kukidhi uhitaji halisi katika kampasi ya Kilimani. Hali hii inatokana na kuwa SUZA ilikipokea kilichokuwa Chuo cha Habari kikiwa katika hali ya ukosefu wa majengo ya kudumu yenye kukidhi hadhi ya Chuo Kikuu na kuwa fedha za ukarabati zilizopendekezwa na Kamati ya Ushauri hazikutolewa.

(b) Upungufu wa wahadhiri wenye sifa hasa kwenye Idara ya Habari, wahadhiri hao ni kwenye somo la “Photo Journalism” na “TV Productions”.

(c) Uhitaji mkubwa wa ukarabati wa miundombinu kwenye Kampasi ya Kilimani.

(d) Uhitaji wa Maabara zenye ubora wa Kompyuta kwa ajili ya kusomeshea.

(e) Uhitaji wa wafanyakazi wenye sifa kwenye kada ya Radio F.M.

(f) Ubadilishaji wa urushaji wa matangazo ya Radio Habari FM kutoka masafa mafupi kwenda masafa marefu kutokana na ukuaji wa Chuo.

(g) Kushindwa kufanya manunuzi ya aina yoyote mpaka waombe fedha na wapate ridhaa ya matumizi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaushauri Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kutenga fedha kwa ajili ya kuanza mradi wa ujenzi wa

majengo ya Skuli ya Kompyuta, Mawasiliano na Mafunzo ya Habari katika eneo walilopatiwa na Serikali hapo awali kabla ya kuunganishwa ili waondokane na uchakavu wa majengo pamoja na miundombinu iliyopitwa na wakati katika kujifunzia na kufundishia.

(b) Kamati inapendekeza kwa Serikali itakapotoa nafasi za ajira kwa Skuli zilizopo chini ya usimamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kulipa kipaumbele suala la uajiri wa wataalamu wa kada zinazohitajika katika Skuli hiyo, ili kuendana na mahitaji halisi ya wakati uliopo wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano.

(c) Kamati inakishauri Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kutafuta wafadhili kwa lengo la kusaidia ununuzi wa vifaa vya maabara za Kompyuta za kufundishia na kujifunzia wanafunzi katika Tasnia ya Mawasiliano na Habari.

(d) Kamati inapendekeza kwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kuwapatia bajeti ya matumizi kwa wakati Skuli zote zinazokusanya mapato kupitia vyanzo vyake vya ndani na hatimae fedha hizo kuingia kwenye 'Account' ya SUZA, ili kuweza kutekeleza makujumu yao ipasavyo waliojipangia kwa bajeti husika pamoja na kuweza kufanya manunuzi kwa vifaa vinavyohitajika kwa wakati.

(e) Kamati inaipongeza Skuli kwa Wahitimu wa Programu za Kompyuta ya Sayansi na TEHAMA kupata ajira mara tu wanapomaliza masomo.

## D. SKULI YA BIASHARA TAWI LA SUZA CHWAKA

Skuli ya Biashara Chwaka ni miongoni mwa skuli zilizo chini ya Tawi la SUZA baada ya kuunganishwa na Chuo hicho mnamo mwaka 2020.

### CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA BIASHARA TAWI LA SUZA CHWAKA

(a) Kuchelewa kuingizwa kwa bajeti kwa ajili ya uendeshaji shughuli za Skuli ya Biashara hali inayosababisha uwepo wa madeni makubwa ambayo Uongozi wa Skuli hiyo unadaiwa.

(b) Kutokuwepo kwa fedha yoyote inayorudi Skuli inayotokana na makusanyo yao ya ndani, hali inayopelekea Skuli kuzorota katika kutoa taaluma zinazolengwa kupatikana na Kamati ilipohoji ilipatiwa taarifa kwamba fedha zote zinazokusanya zinaingizwa kwenye 'Account' ya SUZA.

(c) Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa walimu na wanafunzi ambapo inapelekea walimu kuchelewa kuanza kwa vipindi na wanafunzi kupungua idadi ya kujiunga na Skuli hiyo kutokana na masafa ya maeneo wanayoishi walimu na wanafunzi.

(d) Uchakavu wa jengo la dakhalia wanayoishi wanafunzi wa kike na kiume kwa pamoja ambapo jengo hilo limejengwa kwa miaka ya karibuni na deni la ujenzi huo bado halijamaliza kulipwa kwa ZSSF na cha kushangaza jengo hilo haiba yake imeshapotea kwa kuharibika baadhi ya vifaa.

(e) Ukosefu wa vitendeakazi vya kujifunzia kwa wanafunzi madarasani pamoja na vya kufundishia, ambapo Kamati ilipofanya ziara ilijionea

baadhi ya madarasa hayana vikalio, Maabara ya kompyuta nyingi ni mbovu, hali inayosababisha walimu kuhama na kwenda vyuo vyengine.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaushauri Uongozi wa SUZA kuingizia fedha za bajeti kwa wakati Skuli ya Biashara Tawi la SUZA Chwaka kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbali mbali za Skuli hiyo kama ilivyojipangia katika mwaka wa bajeti husika.

(b) Kamati inapendekeza kwa Uongozi wa SUZA kurejesha kiwango cha fedha kwa Skuli zote zinazokusanya kupitia vyanzo vyake vya ndani zilizopo chini ya usimamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa ikiwemo Skuli ya Biashara Chwaka kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, kwani Kamati imepata taarifa kwamba fedha zinazokusanywa hutumika kwa ajili ya matumizi ya Chuo Kikuu cha Taifa SUZA na badala yake wao kubaki katika hali ya ukosefu wa fedha za uendeshaji wa Skuli hizo.

(c) Vile vile, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Uongozi wa SUZA kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la ukosefu wa usafiri kwa walimu pamoja na wanafunzi wanaoishi katika dakhalia ya Skuli ya Biashara ili kuwaondolea usumbufu kwa walimu na wanafunzi hao wakati wanapopata changamoto za kiafya hususan katika nyakati za usiku.

(d) Kamati inapendekeza kwa Serikali kuwatumia Wakala wa Majengo ya Serikali (ZBA) kwa ajili ya kulihami jengo la dakhalia ya Skuli ya

Biashara Chwaka kabla halijaleta madhara au maafa kwa wanafunzi wanaoishi katika jengo hilo.

(e) Kamati inaishauri Serikali inapotekeleza ujenzi wa miradi mengine inayohusu elimu kulipa kipaumbele suala la ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi wa kiume katika Skuli ya Biashara Chwaka, kwani kwa sasa dakhalia hiyo iliopo wanaishi wanafunzi wanawake na wanaume kwa pamoja hali inayoweza kupelekea mmomonyoko wa Maadili.

(f) Kamati inaipongeza SMT chini ya Uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kukipatia Chuo Kikuu cha Taifa SUZA USD Milioni 10 kupitia Mradi wa HEET (High Education for Economic Transformation).

## 2.5PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI

Programu hii ina lenga kutoa na kuimarisha Elimu ya Sekondari kwa kuhakikisha vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya mitihani ya taifa kwa skuli zote za Sekondari zenye kidatu cha nne na sita vinanunuliwa na kusambazwa katika skuli hizo. Aidha, Programu Kuu hii kwa mwaka 2022/2023 imepangiwa kutumia jumla ya Tanzania shilingi Bilioni Mia Moja na Kumi na Nne, Milioni Arobaini na Tatu, Laki Nane na Sitini na Tano Elfu (114,043,865,000/=).

### A. SKULI YA SEKONDARI YA UFUNDI MIKUNGUNI

Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni ni moja miongoni mwa skuli kongwe hapa Zanzibar ambayo ilianzishwa mwaka 1955 kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo ilikuwa na wanafunzi kumi na nne (14)

wote wa kiume na mwalimu mmoja wa kiume. Aidha, Skuli hiyo mwanzo ilikuwa katika jengo la Skuli ya Ben Bella ambapo ilipatiwa vyumba viwili vya kufanyia mafunzo ya vitendo kuhusu masuala ya mbao (woodwork). Wanafunzi walioingia hapo ni wale walioshindwa kuendelea na masomo ya sekondari. Skuli wakati huo ilikuwa ikiongozwa na Bwana Ali Uki Dahoma ambaye alikuwa ndiye Mwalimu Mkuu wa mwanzo.

Vile vile, Skuli hiyo kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar ilihamia eneo la Mikunguni ambapo Skuli hiyo hivi sasa ndipo ilipo pamoja na kubadilishwa jina na kuitwa Karimjee Trade School na baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ikabadilishwa jina tena na kuitwa Mikunguni Trade School.

Mwaka 1975 Skuli hiyo ikaitwa Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni, ambapo jina hilo ndilo linalotumika mpaka hivi sasa. Skuli hiyo ina jumla ya wanafunzi 283, wanaume 159 na wanawake 124 ambao wamegaiwa katika idara tano za Computer, Mechanics, Civil, Umeme na Electronics.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA SEKONDARI YA UFUNDI MIKUNGUNI

(a) Mashine za Idara ya ‘Mechanics’ ni kongwe sana na pia zimekuwa chache kwa kuharibika mara kwa mara.

(b) Ukosefu wa Dakhalia ya wanafunzi wa kiume, hali inayosababisha wanafunzi kuishi katika mazingira magumu hivyo kushindwa kufikia malengo waliojiwekea katika masomo yao.

(c) Ukosefu wa usafiri kwa wanafunzi, hali inayopelekea kuzorota kwa utekelezaji wa majukumu wakati wanafunzi wanapohitaji kwenda kufanya mafunzo ya kujifunza katika Taasisi tofauti za Serikali.

(d) Uhaba wa watendaji hali inayokwaza utekelezaji wa kazi za skuli kwa ufanisi, ambapo walimu wengi wa Kiwanda cha Ufundi Seremala na Sehemu ya Ufundi wa ‘Welding’ wamestaafu na hakuna wataalamu wapya walioajiriwa.

(e) Uzio wa Skuli haujakamilika, hali hiyo inasababisha wahalifu kuweza kuingia katika maeneo ya Skuli hiyo na kufanya matukio ya uhalifu pamoja masuala ya udhalilishaji.

(f) Baadhi ya wanafunzi wanaomaliza masomo yao katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kushindwa kuendelea na masomo katika Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KITS) kutokana na gharama za malipo ya masomo katika Taasisi hiyo kuwa kubwa na ukizingatia hali za maisha yao ni duni.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulitafutia ufumbuzi suala la ukosefu wa baadhi ya mashine muhimu za kufundishia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kwa ajili ya kuweza kupata ujuzi na taaluma ya ufundi, ili wanafunzi hao wanapomaliza

masomo yao waweze kuendelea na vyuo vyengine kwa masomo na hatimae kujiajiri wenyewe au kuajiriwa.

(b) Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kuanzisha Dakhalia ya wanafunzi wa kiume kwani hivi sasa ipo Dakhalia ya wanafunzi wanawake pekee, hali ambayo inapelekea baadhi ya wanafunzi wanaume kuishi katika mazingira magumu.

(c) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuipatia Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni usafiri wa kudumu kwa ajili ya wanafunzi ili waweze kuondokana na changamoto hiyo hasa pale wanapopangiwa kufanya mafunzo ya vitendo katika taasisi nyengine zilizopo nje ya maeneo ya skuli.

(d) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wakati inapotangaza nafasi za ajira ni vyema kuzingatia uajiri wa wataalamu wenye fani na taaluma zinazohitajika katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni ili kuondoa kadhia ya ukosefu wa wataalamu wa masomo mbali mbali katika Skuli hiyo.

(e) Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kuukamilisha ujenzi wa uzio wa Skuli hiyo kwa lengo la kuzuia wahalifu wasiingie ndani ya eneo hilo la skuli pamoja na kuwajengea wanafunzi wetu kuishi katika mazingira mazuri na yaliosalama kwao.

(f) Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kuweka utaratibu maalum kwa wanafunzi wanatoka Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni kuweza kuendelea na masomo yao katika Taasisi ya

Karume ya Sayansi na Teknolojia (KITS) kwa kuwapunguzia gharama za malipo ya masomo ili nao waweze kutimiza ndoto zao za kuendelea na masomo yao ya sayansi, kwani hivi sasa Zanzibar ina uhaba wa wataalamu wa masuala ya ufundi.

## B. CHUO CHA KIISLAMU PEMBA (CCK)

Chuo cha Kiislamu Pemba kina majukumu ya kutoa mafunzo ya ualimu kwa walimu watarajiwa (Pre - Service) kwa ngazi ya cheti na stashahada za msingi na sekondari kwa masomo ya Sayansi, Dini/Kiarabu na Sanaa kwa ujumla. Mafunzo hayo yanatolewa kwa lengo la kupata walimu mahiri na wenye uwezo wa kutoa taaluma sahihi kwa wanafunzi. Chuo kina muundo wa Idara Kuu nne nazo ni:

(i) Idara ya Utawala, Mipango na Uendeshaji;
(ii) Idara ya Taaluma;
(iii) Idara ya Huduma za Maktaba; na
(iv) Idara ya Utafiti na Uandishi wa Miradi.

Katika Idara hizi nne (4) zimo Divisheni saba (7) ambazo ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu na malengo ambayo Chuo kimejipangia. Divisheni hizo ni Divisheni ya Usajili na Udahili, Divisheni ya Mitihani, Divisheni ya Mitaala, Divisheni ya Utafiti, Divisheni ya Mipango, Divisheni ya Ustawi wa Wanafunzi pamoja na Divisheni ya Rasilimali Watu. Kwa sasa chuo kina jumla ya wanafunzi 416, wakufunzi 24 na wafanyakazi 16 wasiokuwa walimu.

**CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI CHUO CHA KIISLAMU PEMBA**

(a) Kumekuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wanojiunga katika mafunzo ya ualimu kwa upande wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Diploma ya Dini na Kiarabu.

(b) Kukosekana kwa mazingira bora ya kujifunzia kutokana na upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia hasa katika maabara za masomo ya Sayansi, TEHAMA na Maktaba.

(c) Ufinyu wa makaazi ya wanafunzi. Hivi sasa Chuo kina mabweni matatu (3) yenye uwezo wa kulala wanafunzi 240 tu ambapo wanaohitaji huduma hiyo kwa sasa ni 675 wakiwemo wanafunzi wa sekondari.

(d) Uchache wa nyumba za walimu, kwa sasa zipo nyumba mbili (2) za familia nne (4) ambapo wanaohitaji huduma hiyo ni zaidi ya familia kumi (10).

(e) Uchache wa madarasa.

(f) Majengo mengi ya madarasa na dakhalia yanavuja wakati wa vipindi vya mvua.

(g) Upungufu wa wafanyakazi kama vile walinzi , mtunza maabara, wakutubi, mshika fedha, wahudumu, katibu mukhtasi, ‘metron’, wapishi na mtunza ghala.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inashauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuandaa utaratibu wa upatikanaji

wa wataalamu wa afya katika Dakhalia za Chuo cha Kiislamu Pemba. Kwani Kamati imebaini kuwa wanafunzi wanaoishi ndani ya Chuo wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa wataalamu wa afya pale inapotokezea mwanafunzi kupata tatizo la kiafya wakati wa usiku na kukosekana kwa huduma hizo katika mazingira ya Chuo.

(b) Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa walimu pamoja na wanafunzi ili kuweza kuondokana na changamoto ya walimu kuchelewa kuanza kwa vipindi vya masomo pamoja na kupunguza uchelewaji wa wanafunzi madarasani.

(c) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya marekebisho ya Mtaala wa Vyuo vya Ualimu vilivyopo nchini ili kuweza kwenda sambamba na mahitaji ya mabadiliko ya mifumo ya elimu nchini.

(d) Kamati inaendelea kupendekeza kwa Serikali kuwepo kwa posho la mazingira magumu kwa walimu wote wanaosomesha katika maeneo ambayo hakuna usafiri wa uhakika.

(e) Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango Mkakati wa uhamasishaji wa wanafunzi kujiunga na mafunzo ya ualimu kwa upande wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Diploma ya Dini na Kiarabu ili kupunguza uhaba wa walimu wa kada hizo katika Vyuo vyetu.

(f) Kamati inaiomba Serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika maabara zetu za masomo ya sayansi, TEHAMA pamoja na maktaba.

(g) Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la uvujaji wa madarasa pamoja na majengo ya dakhalia wanayoishi wanafunzi, hali inayopelekea kutokuwepo kwa mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia.

## 2.6 PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Kimsingi Programu hii imeundwa na Programu Ndogo Moja ambayo inalenga kusimamia elimu bora katika ngazi zote za elimu na kutoa huduma za Kuandaa Mitaala na Kuratibu Uandaaji wa Vitabu na Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia, Kutayarisha na Kusimamia Mitihani, Ukaguzi katika ngazi ya Elimu ya Skuli na katika Mfumo wa Elimu, Kutoa Taaluma ya Habari na Mawasiliano, ili itumike kama nyenzo ya Kufundishia na Kujifunzia, Kusajili Skuli na Kutoa Leseni za Walimu, Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Kutoa fursa kwa jamii kujisomea na kutafuta taarifa za kielimu na kuibua vipaji vya michezo kwa wanafunzi.

Lengo kuu la kuwepo huduma hizi ni kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa katika ngazi zote za elimu ni yenye ubora kwa manufaa ya wenye kuhitimu, jamii na Taifa kwa ujumla.

### A. OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR

Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu (OICE) ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya Sheria Nam. 10 ya mwaka 2018. Aidha, Ofisi inasimamiwa na Bodi ya Ushauri ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu iliyoundwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Mkaguzi

Mkuu wa Elimu. Jukumu kuu la Ofisi hii ni kusimamia ubora wa elimu nchini.

Vile vile, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu katika kusimamia Ubora wa Elimu hufanya ukaguzi wa elimu kwa skuli zote za Maandalizi, Msingi na Sekondari zilizosajiliwa pamoja na Taasisi zinazotoa Mafunzo ya Ualimu, Vyuo vya Elimu Mbadala, Elimu ya Watu Wazima, Taasisi za Elimu zilizosajiliwa zilizo nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU ZANZIBAR**

(a) Ukosefu wa Majengo ya Ofisi, kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzishwa kwa Ofisi ambapo imeanzisha ndani ya Ofisi za Ukaguzi za Mikoa. Ofisi hizi kwa sasa zipo kinadharia tu. Wakaguzi wamegawiwa kimkoa na wanatekeleza majukumu yao kwa mgawanyiko wa mikoa, hata hivyo kiutendaji Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini Unguja wapo katika jengo la Ofisi kuu ambalo halina nafasi. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wamepewa chumba kimoja katika majengo ya Ofisi ya SUZA Beit-El-Ras.

    Kwa upande wa Pemba, Wakaguzi wa Mkoa wa Kusini wapo Chake Chake katika jengo la Huduma za Maktaba, na wakaguzi wa Mkoa wa Kaskazini wapo katika jengo la Ofisi ya Elimu Mkoa wa Wete.

(b) Uhaba wa usafiri wa uhakika kwa Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu, hali hiyo inapelekea kuzorota utekelezaji wa majukumu kwa Ofisi hiyo na kushindwa kufikia malengo iliyojipangia wakati, ambapo kwa muda

mwengine wakaguzi hutumia usafiri binafsi na wa kawaida na wakati mwengine huazima gari za Wizara kwa ajili ya kuweza kusaidia kutekeleza majukumu yao.

(c) Upungufu wa watendaji ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ilikuwa na jumla ya watendaji 88 (28 – Pemba na 60 - Unguja) kati ya hao wakaguzi ni 72, Karani Masjala mmoja (1), Afisa Utumishi mmoja (1), Katibu Mhutasi (1), Afisa Takwimu mmoja (1), Afisa Teknolojia ya Mawasiliano mmoja (1), Mshika Fedha mmoja (1), Wahudumu wawili (2) Unguja, Walinzi watatu (3) Unguja, Dereva watatu (3) na Mwangalizi wa Ofisi mmoja (1). Idadi hiyo ya watendaji bado haijakidhi mahitaji ya Ofisi, ikizingatiwa uhitaji wa kuwepo kwa Ofisi za Ukaguzi za Mikoa na mahitaji ya muundo wa Ofisi. Hivyo, kuna haja ya upatikanaji kwa watendaji ili kukidhi mahitaji ya muundo mpya wa Ofisi.

(d) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu katika kufanya kazi zake za ukaguzi haiendani na Muongozo wa Ufikiwaji wa Miundombinu Rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu katika skuli zetu zinazosomesha Elimu Mjumuisho katika ngazi ya Elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwatengea bajeti maalum kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu pamoja na Ofisi za Wakaguzi wa Elimu

Mikoa ili kuweza kufikia malengo ya kuanzishwa kwa ofisi hizo kila mikoa kwa Unguja na Pemba.

(b) Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar katika bajeti ya mwaka 2023/2024, suala la upatikanaji wa usafiri wa kudumu kwa Ofisi hiyo kupewa kipaumbele kwani kubaki kama ilivyo sasa inapelekea wakaguzi kupata ugumu wa kusimamia ubora wa elimu katika skuli zetu.

(c) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora zinapotangazwa nafasi za ajira mpya kwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kuweza kuzingatia mahitaji ya kada zinazohitajika kwa ajili ya kufikia azma ya Serikali ya kukuza elimu nchini.

(d) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuliandalia utaratibu mzuri suala la ukaguzi wa elimu katika skuli zetu za Elimu Mjumuisho kuanzia ngazi ya Elimu ya Maandalizi, Msingi na hata Sekondari ili nao waende sambamba na mabadiliko ya Sekta ya Elimu Zanzibar.

## B. BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR

Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar ilianzishwa chini ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 1993. Bodi ya Huduma za Maktaba ni Taasisi kongwe ambayo imeanza kazi zake za utoaji wa huduma kuanzia mwaka 1988 kwa Unguja na mwaka 1994 kwa upande wa Pemba. Kwa sasa Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar ina jumla ya ofisi/matawi manne (4), ambapo mawili yapo Unguja na mawili Pemba.

Aidha, Bodi ya Huduma za Maktaba inalenga zaidi kutoa huduma bora za Maktaba kwa jamii nzima ili kusaidia juhudi za Serikali katika kuinua kiwango cha elimu pamoja na kuleta maendeleo katika nyanja zote za maisha kwa kuweka misingi imara ya upatikanaji wa elimu na taarifa kwa umma.

Majukumu ya Bodi ya Huduma za Maktaba kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) cha Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba ya mwaka 1993, Bodi ina majukumu yafuatayo:

(a) kuanzisha, kukuza na kuendeleza Huduma za Maktaba katika Visiwa vya Zanzibar;
(b) kuhakikisha upatikanaji wa vitabu na machapisho mengineyo kutoka kwa waandishi mbali mbali wa ndani na nje ya Zanzibar;
(c) kuanzisha, kusimamia na kuendeleza Maktaba za Umma katika ngazi za Mikoa na Wilaya;
(d) kuanzisha, kusimamia na kuendeleza Maktaba Ndogo Ndogo katika Taasisi mbali mbali, jamii na skuli;
(e) kuwezesha upatikanaji wa nyenzo na vifaa vya kufanyia kazi katika Maktaba za Umma;
(f) kujenga mazingira mazuri kwa watumiaji wote wakiwemo watu wenye mahitaji maalum katika maeneo yote yanayotoa huduma za maktaba;
(g) kutoa usajili wa kuanzisha Maktaba za Jamii, skuli na taasisi mbali mbali;
(h) kuongeza kiwango cha elimu kwa jamii ili kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika;

(i) kukusanya Ripoti za Utafiti na kuhifadhi katika Maktaba kwa ajili ya kutumika kama kumbukumbu kwa watafiti wengine;

(j) kutoa elimu na maarifa juu ya utoaji na usimamiaji wa huduma za Maktaba.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA**

(a) Uhaba wa wataalamu hasa wakutubi na maafisa waendeshaji katika Maktaba zetu za Unguja na Pemba.

(b) Tatizo la usafiri kwani Ofisi ina gari mbili moja Unguja na moja Pemba na haziko kwenye hali nzuri hivyo kushindwa kufuatilia na kutekeleza majukumu yao ya Ofisi kwa ufanisi mzuri.

(c) Uwepo wa miundombinu chakavu ya jengo na uhaba wa nafasi.

(d) Tatizo la uhaba wa vitendeakazi hasa vifaa vya TEHAMA na vifaa vya kuendeshea programu za maktaba hususan watu wenye ulemavu na watoto.

(e) Uchache wa vitabu ndani ya maktaba hali inayopelekea wanafunzi kushindwa kupata baadhi ya vitabu kwenye maktaba ambazo ziko karibu na maeneo yao na kupelekea kuvifuata masafa marefu na wakati mwengine kuvikosa kabisa.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati imefurahishwa na utaratibu wa uhamasishaji wa jamii katika kutoa taaluma kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba kwa kushiriki kwenye Maonesho mbali mbali pamoja na Mitandao ya Kijamii.

(b) Kamati inashauri Serikali kulipatia ufumbuzi suala la uchache wa wataalamu katika Bodi ya Huduma za Maktaba kwa kutoa kibali cha uajiri ili huduma zitolewe kwa ufanisi zaidi.

(c) Kamati inapendekeza kwa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa mpango Madhubuti wa ununuzi wa vifaa kwa Bodi ya Huduma za Maktaba pamoja na kuwawekea miundombinu rafiki wanafunzi pamoja na watu wenye ulemavu ili waweze kunufaika na huduma zinazotolewa na Maktaba hizo.

(d) Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Bodi ya Huduma za Maktaba kuifanyia marekebisho Sheria Nam. 7 mwaka 1993 ya Bodi ya Huduma za Maktaba, kwani Sheria hiyo imekuwa na mapungufu mengi na haina Kanuni ya kusaidia utekelezaji wa Sheria hiyo.

(e) Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea bajeti Bodi ya Huduma za Maktaba, kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa ufanisi.

(f) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwapatia usafiri Bodi ya Huduma za Mkataba.

(g) Kamati inaitoa wito kwa jamii kujiunga na Bodi ya Huduma za Maktaba kwa ajili ya kuweza kupata taaluma mbali mbali ikiwemo vitabu vya fani tofauti kwa lengo la kujiongezea maarifa, elimu ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya elimu nchi.

## C. SKULI YA MSINGI YA MICHAKAINI PEMBA

Skuli ya Michakaini ni miongoni mwa skuli nane (8) za mwanzo za Elimu Mjumuisho zilizoanzishwa mwaka 2005 kwa Pemba baada ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuanzisha rasmi Mfumo wa Elimu Mjumuisho Zanzibar. Skuli hii imekuwa ikidakhili wanafunzi mbali mbali wenye mahitaji maalum wakiwemo wenye ulemavu. Skuli hii tayari imeweza kuwapatia elimu wanafunzi mbali mbali wenye ulemavu na baadhi yao kuweza kufika ngazi ya elimu ya juu. Aidha, wanafunzi wawili wenye ulemavu wasioona ambao walianza darasa la kwanza 2006 mara tu baada ya kuanzishwa Mfumo wa Elimu wa Mjumuisho katika Skuli ya Michakaini wanaendelea na masomo katika ngazi ya Shahada ya Kwanza kwa fani ya Ustawi wa Jamii Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU).

Skuli ya Michakaini pamoja na utekelezaji wa elimu mjumuisho, pia ina vituo viwili ambavyo vinashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa akili na kituo cha kupima na kuwatambua wanafunzi wenye usikivu hafifu. Baada ya kutambuliwa wanafunzi wenye usikivu hafifu na wataalamu waliopo hapo hupelekwa katika hatua nyengine ili kushughuliwa zaidi ama kwa kupatiwa shime sikio au hatua nyengine za kimatibabu ili waweze kuendelea vyema na masomo yao.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SKULI YA MSINGI YA MICHAKAINI PEMBA

(a) Uchakavu wa majengo hali inayopelekea wanafunzi na walimu kuwa katika mazingira hatarishi.

(b) Uhaba wa madarasa ya kufundishia na kujifunzia wanafunzi hali inayowasababishia kuingia mikondo miwili na wengine kusoma chini ya miti na mpaka msikitini.

(c) Kuwepo kwa posho dogo kwa walimu wanaowashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa akili, uoni na usikivu hafifu.

(d) Kukosekana kwa mafunzo maalum kwa walimu wanaosomesha wanafunzi wa Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha.

(e) Uhaba wa vifaa na vitabu vya kufundishia na kujifunzia kwa walimu na wanafunzi waliopo katika skuli hiyo ikiwemo brille mashine, stick, miwani ya kusomea na kompyuta.

(f) Kutokuwepo kwa miundombinu rafiki na yenye kufikika katika mazingira ya skuli hiyo.

(g) Kutokuwepo kwa idadi halisi ya wanafunzi wenye ulemavu wanaohitimu na kuendelea na masomo katika ngazi nyengine za Elimu hadi ngazi ya elimu ya juu kwa vyuo vikuu vya ndani na nje.

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(a) Kamati inaishauri Serikali kwa mwaka wa fedha unaokuja kutenga fedha maalum za ujenzi wa skuli ya Msingi mpya ya Michakaini Pemba kwani kwa sasa skuli hiyo imekuwa chakavu na haikidhi

mahitaji yaliopo kwa kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi wapatao 4200 ikijumuisha na elimu mjumuisho.

(b) Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Kitengo cha Elimu Mjumuisho kuwapatia mafunzo ya Lugha za Alama kwa walimu wanaoshughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa aina hiyo ili waweze kuendaa na mabadiliko ya Mitaala ya Elimu.

(c) Kamati inashauri Serikali katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kuwaongezea posho la mazingira magumu kwa walimu wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu kwa Unguja na Pemba kwa ajili ya kuwaongezea ari ya kufanya kazi.

(d) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuufuata na kuutekeleza kwa vitendo Muongozo uliotolewa na Serikali wa mwaka 2016 kuhusu miundombinu rafiki na inayofikika kwa watu wenye ulemavu katika majengo yote ya Serikali yanayoendelea kujengwa ikiwemo skuli zetu za Maandalizi, Msingi pamoja na Sekondari.

(e) Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kukaa pamoja na Kitengo cha Elimu Mjumuisho kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la ukosefu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa skuli zenye kusomesha Elimu Mjumuisho ili kufikia azma ya Serikali ya utoaji wa elimu bora kwa wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

## 2.7 PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Lengo la Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ni kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali bora na usimamizi mzuri wa matumizi yake katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mbili na Tisiini na Nane Elfu (17,002,098,000/=) zitumike kupitia Programu Ndogo Tatu nazo ni Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara pamoja na Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wizara Pemba.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

(a) Kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha katika ujenzi wa miradi yote inayotekelezwa kupitia fedha za UVIKO 19 hali iliyopelekea Wizara kuongeza fedha za ziada (variations) Tanzania Shilingi Bilioni 15 mbali na fedha za awali walizopatiwa kiasi cha Tanzania Shilingi Bilioni 68 ili kufanikisha ujenzi wa miradi hiyo.

(b) Uhaba wa fedha za Mikopo kwa wanafunzi waliojiunga na Elimu ya Juu hasa wanaosoma nje hali inayowapelekea baadhi ya wakati kuzuiwa kufanya mitihani yao au kusimamishwa kuendelea na masomo.

(c) Uhaba wa walimu wa Sayansi katika skuli zote za Unguja na Pemba. Mfano halisi, Skuli ya Mkwajuni kwa mwaka huu Wizara imeanzisha darasa la michipuo ila walimu wa Sayansi katika Skuli hiyo hakuna.

(d) Kuwepo kwa ongezeko kubwa la idadi ya walimu wasiothibitishwa kwa kupatiwa leseni za kufundisha.

(e) Kutokuwepo kwa vitabu vya mitaala katika skuli za Serikali hali inayopelekea ufaulu mdogo wa wanafunzi hususan kwa wanafunzi wa sayansi.

(f) Kuondolewa kwa somo la Dini na Kiarabu kwa mwaka huu kwa wanafunzi waliofanya mtihani wa Darasa la Nne wakati katika mtaala wa kusomeshwa masomo hayo yapo.

(g) Kutokuwepo kwa maeneo maalum ya kusahihishia mitihani hali inayopelekea Baraza la Mitihani kukodi maeneo ya watu binafsi kwa fedha nyingi na yasio salama kwa ajili ya kusahihishia mitahani kinyume na matakwa ya Sheria ya Kuanzisha Baraza hilo.

(h) Kuchelewa kupatikana kwa vibali vya ajira kwa nafasi za ajira mpya hali inayosababisha uhaba wa walimu katika maeneo yote ya Unguja na Pemba.

(i) Kupanga kwa makadirio makubwa ya Mapato ya Wizara kinyume na hali halisi ya makusanyo ya Mapato hayo.

(j) Kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika kwa wakaguzi wakati wanapokwenda kufanya ukaguzi katika Skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari hasa katika skuli zilizopo kwenye visiwa.

(k) Posho dogo kwa wakaguzi wetu wa ndani wanaokwenda kufanya ukaguzi katika skuli zilizopo kwenye visiwa kama vile Fundo, Kokota, Kojani, Tumbatu, hali inayowasababishia kukaa dago kwa ajili ya kutekeleza shughuli zao za ukaguzi.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kuunda Kamati Maalum ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mikataba inayoingiwa baina ya Serikali yetu na Wakandarasi mbali mbali kwa lengo la kujenga usimamizi imara na madhubuti kwa wataalamu wetu wa ndani.

(b) Kamati pia inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi kubwa walizochukua katika kufanya ukarabati na ujenzi wa Madarasa na Majengo ya Ghorofa ya kisasa Skuli mbali kwa Unguja na Pemba katika kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira rafiki na salama.

(c) Kamati inaishauri Wizara inapotekeleza Miradi ya Maendeleo katika Sekta yoyote lazima kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa Taasisi husika ili kuepusha changamoto ya upotevu wa fedha za Serikali.

(d) Kamati pia inaishauri Serikali kwa Kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuipunguza mzigo Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara kushughulikia na kusimamia miradi yote ujenzi kwa kurudisha Idara ya Ujenzi kama ilivyo kuwa awali kwa lengo la kupunguza changamoto zinazojitokeza za matumizi makubwa ya fedha za ziada (variations) kinyume na utaratibu uliopo kisheria.

(e) Kamati inashauri Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kusomesha wanafunzi katika vyuo vyetu vya ndani hasa kwa “Course” zinazopatikana ndani badala ya kutumia fedha nyingi za kugharamia wanafunzi kwenda vyuo vya nje na kutilia mkazo fani zinazoendana na Sera ya Uchumi wa Buluu.

(f) Kamati inaishauri Serikali pamoja na Wizara kabla ya kuanza kwa ujenzi wa miradi yoyote kufanyike upembuzi yakinifu wa maeneo

yanayokwenda kujengwa mradi kabda ya kuanza kwa ujenzi ili kuipunguzia Serikali matumizi ya ziada.

(g) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwapatia mafunzo kila baada ya muda wahandisi wetu wa ndani wa Wizara pamoja na Watu wa Manunuzi kwani Kamati imegundua kuwa ongezeko lililojitokeza katika miradi hii mikubwa ya ujenzi wa skuli umechangiwa kwa kiasi kikubwa na wasimamizi wetu kutokuwa na utaalamu wa kutosha katika masuala ya usimamizi wa miradi mikubwa na mingi kwa wakati mmoja.

## 3. WIZARA YA AFYA

Kamati katika kipindi chote cha kazi zake imefanyakazi ya kusimamia utekelezaji wa bajeti inayotumia muundo wa programu katika utekelezaji wake, ambapo kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara hii ilitekeleza na programu zifuatazo:

*(i)* Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya;
*(ii)* Programu Kuu ya Huduma za Tiba;
*(iii)* Programu Kuu ya Uratibu na Uendeshaji wa Wizara ya Afya; na
*(iv)* Programu Kuu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Programu hizo zinatekelezwa kupitia Wizara ya Afya ambapo jumla ya Idara Tano (5), Taasisi Tano (5) na Mabaraza saba (7) ya Taaluma mbali mbali za Kiafya kama ifuatavyo:

### 3.1IDARA

*(i)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
*(iii)* Idara ya Kinga na Elimu ya Afya;
*(iv)* Idara ya Mfamasia Mkuu wa Serikali;
*(v)* Idara ya Bohari Kuu ya Dawa; na

## 3.2TAASISI

*(i)* Hospitali ya Mnazi Mmoja;
*(ii)* Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi;
*(iii)* Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;
*(iv)* Maabara ya Afya ya Jamii - Pemba; na
*(v)* Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar.

## 3.3MABARAZA YA KITAALUMA/BODI

*(i)* Baraza la Wauguzi na Wakunga;
*(ii)* Baraza la Madaktari;
*(iii)* Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala;
*(iv)* Baraza la Afya ya Jamii;
*(v)* Baraza la Wataalamu wa Afya ya Mazingira;
*(vi)* Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya; na
*(vii)* Bodi ya Ushauri wa Huduma za Hospitali Binafsi.

Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hizo, Kamati ilifanya ziara katika Hospitali na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuona mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Programu zilizopangwa pamoja na kubaini changamoto mbali mbali zinazokwamisha utekelezaji wa shughuli katika sehemu hizo na kuziwasilisha Serikalini kwa kuishauri Serikali namna bora itakayoweza kutumika katika kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

## 3.4PROGRAMU KUU YA KINGA NA ELIMU YA AFYA

Jukumu la Programu hii ni kuhakikisha kwamba jamii inapata huduma bora za kinga pamoja na kuongeza uelewa juu ya njia sahihi za kujikinga na maradhi ya kuambukuiza na yasiyoambukiza. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha Tanzania shilingi Bilioni Thelathini na Nne, Milioni Mia Nne na Kumi, Laki Moja na Kumi na Tatu Elfu (34,410,113,000/=) zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za programu hii.

### A. DIVISHENI YA AFYA YA AKILI HOSPITALI YA KIDONGO CHEKUNDU

Divisheni ya Huduma za Afya ya Akili Hospitali ya Kidongochekundu ni Hospitali Maalum inayotoa huduma kwa wananchi wa Zanzibar wanaosumbuliwa na matatizo ya Afya ya Akili. Divisheni hii inatoa huduma ikiwemo:

(a) Huduma za wagonjwa wa nje (OPD);
(b) Huduma za wagonjwa maalum wanaotumia methadone (MAT clinic);
(c) Huduma za kulaza:

   (i) Wagonjwa wa kawaida,
   (ii) Watoto na vijana,
   (iii) Wagonjwa waliopata uraibu (addiction).

Aidha, divisheni hii ina malengo yafuatayo:

(a) kutoa huduma za matibabu ya afya ya akili;
(b) kuimarisha huduma za afya ya akili kwa wagonjwa wanaohudhuria ikiwemo kutoa elimu kwa jamii inayotuzunguka;
(c) kujenga tabia ya kujifunza na kupeana ujuzi kwa wafanyakazi wa divisheni pamoja na wanafunzi.

Vile vile, divisheni hii pia ina majukumu kadhaa ambayo ni pamoja na:

(a) kuendesha kliniki ya wagonjwa wenye magonjwa ya akili;
(b) kutoa matibabu na ushauri wa kisaikolojia kwa wagonjwa wenye matatizo mbali mbali ya akili. Kwa mfano, sonona, mripuko wa akili, wasi wasi, kukojoa kitandani wakati wa kulala;
(c) kufuatilia wagonjwa waliokuwa wanatumia dawa za kulevya ambao tayari kupata tiba ya kuacha dawa hizo (detox);
(d) kuhakikisha uwepo wa vitendeakazi na vinaendana na viwango, muongozo na taratibu zilizowekwa kwa ajili ya utoaji huduma za divisheni;
(e) kusimamia na kuboresha viashiria vya ndani/nje vya utendaji kazi (KPI) ikiwemo viwango vya huduma bora zilizotolewa ili kuimarisha huduma, kutoa mrejesho juu ya utendaji wao kila wakati;
(f) kusimamia miongozo ya timu ya madaktari wa divisheni; na
(g) Kusimamia wanafunzi wanaokuja kujifunza kwa vitendo katika divisheni.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI DIVISHENI YA AFYA YA AKILI HOSPITALI YA KIDONGOCHEKUNDU

(a) Uhaba wa watendaji hususan Wataalamu Bingwa pamoja na wafanyakazi wengine hali hii inasababisha kuzorota kwa utendaji wa kazi katika divisheni hiyo.

(b) Bajeti ndogo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbali mbali Divisheni hiyo, hali inayopelekea baadhi ya shughuli kutekelezwa nje ya muda uliopangiwa ambapo bajeti kubwa wanayoipata hutokana na fedha za ufadhili kutoka mashirika ya nje na pia haiwatoshelezi kufikia azma ya malengo waliojipangia kutekeleza kwa muda husika.

(c) Mazingira magumu ya kufanya kazi katika Divisheni ya Afya ya Akili ikiwemo kupigwa kwa wauguzi, hali ambayo inawatia hofu wauguzi pamoja na watendaji wengine katika divisheni hiyo.

(d) Uchache wa sare (uniform) kwa watendaji pamoja na wagonjwa hali inayopelekea sare hizo kuvaliwa kwa muda mrefu mpaka kufikia hatua ya kuchakaa.

(e) Kuwepo kwa asilimia kubwa ya watendaji wa mkataba katika Divisheni hii wanaolipwa na wafadhili ambao itakapomaliza programu hiyo divisheni hii itakuwa na upungufu wa wafanyakazi wa kudumu.

(f) Uhaba wa dawa zinatumiwa kwa ajili ya kuwasaidia wagonjwa walioathirika na uraibu.

(g) Kutokuwepo kwa posho la aina yoyote kwa watendaji hao wanafanya kazi katika mazingira hatarishi na magumu.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kukaa na Wizara ya Afya kuliangalia kwa kina suala la ukosefu wa watendaji wa kudumu wa Serikali katika Divisheni ya Afya ya Akili Hospitali ya Kidongo Chekundu ambao wanatoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanaofika hapo kwani Kamati imeshangazwa kuona watendaji waliopo asilimia kubwa wameajiriwa kwa mkataba na kulipwa na Mfadhili kwa kipindi maalum.

(b) Kamati pia inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la kuwaondolea watendaji wa afya posho la mazingira hatarishi (risk allowance) kwa watendaji wa divisheni pamoja na hospitali nyengine.

(c) Kamati inapendekeza kwa Serikali pamoja na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuitengea fungu maalum la fedha za uendeshaji wa Divisheni ya Afya ya Akili Hospitali ya Kidongo Chekundu na sio vyema kutegemea fedha kwa asilimia kubwa kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya uendeshaji wa hospitali hiyo bila ya kutenga fedha yoyote kutoka katika bajeti yetu ya Serikali.

(d) Vile vile, Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu wa kuwaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia nafasi za mafunzo kazini ya muda mfupi na muda mrefu ili kuzalisha wataalamu bingwa wa kada tofauti za afya ikiwemo Afya ya Akili.

## B. KITENGO CHA AFYA YA KAZINI (OHU) PEMBA

Usalama na afya kwa wafanyakazi ni muhimu sana na kunauhitaji pamoja na uangalizi mkubwa na kuwepo kwa mifumo Madhubuti ya kusimamia

usalama na afya kwa wafanyakazi katika sehemu zao za kazi. Miongoni mwa majukumu yao ni kufanya ukaguzi wa afya na mazingira katika sehemu za kazi, kufanya uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi mbali mbali na kuwapatia matibabu kwa wale waliogundulika na magonjwa, kutoa elimu ya afya na maelekezo mbali mbali katika sehemu za kazi kwa wafanyakazi na uongozi kwa ujumla, kujaza fomu za fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali, maambukizi au vifo wakiwa kazini, kuongeza mashirikiano ya kikazi na vitengo vyengine vya ndani na nje ya Wizara ili kuongeza ufanisi wa kazi na kutoa elimu ya afya juu ya matumizi sahihi ya vifaa kinga (PPE) kwa wafanyakazi ili kupunguza ajali na maradhi yanayotokea sehemu za kazi.

**CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KITENGO CHA AFYA YA KAZINI**

(a) Ukosefu wa vitendea kazi kama vile kompyuta mpakato kwa ajili ya uhifadhi wa kumbukumbu na matumizi ya Ofisi wakati wa kazi za nje ya Ofisi.
(b) Kutokuwa na usafiri wa Ofisi kwa shughuli za ukaguzi na ufuatiliaji wa kazi katika maeneo ya mbali na kazi.
(c) Upungufu wa vitendanishi kwa ajili ya maabara inayotumika kwa hospitali.
(d) Ufinyu na uchakavu wa jengo hali inayopelekea wanaohitaji huduma kwenda katika hospitali za binafsi na kuikosesha mapato Serikali.
(e) Kuwepo kwa mashirikiano madogo baina ya Kitengo na Maafisa Utumishi wa Wizara nyengine hususan katika suala zima la upimaji wa afya kwa wafanyakazi wao na ujazaji wa fomu za fidia pale inapotokezea ajali kazini.

(f) Kutokuwa na vitambulisho vya kazi kwa watendaji wa Kitengo cha Afya Kazini hali inayowapelekea wakati wa kufanya ukaguzi katika maeneo kuzuiliwa kuingia au kufukuzwa.

(g) Kutokuwepo kwa ofisi za kudumu katika maeneo yote wanayotumia kwa Unguja na Pemba.

(h) Kutokuwa na bima ya afya kwa wafanyakazi wa Kitengo cha Afya Kazini.

(i) Kutokuwepo kwa gari maalum ya kubebea wagonjwa (Ambulance) katika maeneo yao wanayofanyia kazi pale inapotokezea kumgundua muathirika au mgonjwa wa dharura katika Bandari zetu na Viwanja vya Ndege.

(j) Kuwepo kwa madeni makubwa ya wafanyakazi yanayotokana na muda wa ziada wa kazi (Overtime).

(k) Ucheleweshwaji wa upatikanaji wa kibali cha kuingia (Power of Entry) katika eneo lolote la kazi kwa ajili ya kufanya ukaguzi kwa wafanyakazi wa kitengo katika maeneo ya Serikali na Binafsi.

(l) Kutokuwepo kwa idadi halisi ya wageni wanaotumia Bandari na Viwanja vya Ndege vyetu.

(m) Uchelewaji wa upatikanaji wa kadi za UVIKO – 19 kwa watu wanaofika kwa lengo la kupata huduma ya kuchanja katika kitengo hicho Pemba mpaka zitengenezwe Unguja.

**MAONI/USHAURI NAMAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Kitengo cha Afya Kazini kuharakisha upatikanaji wa vitambulisho vya kazi kwa wafanyakazi wao ili kuwasaidia kutambulika katika maeneo yoyote ya

kazi kwa ajili ya kufanya kazi zao kwa ufanisi bila ya migongano yoyote na waajiri katika Serikali pamoja na Sekta Binafsi.

(b) Kamati inaishauri Serikali katika mipango yao ya mwaka wa fedha 2023/2024, kuwapatia Ofisi Kitengo cha Afya Kazini Pemba pamoja na usafiri wa uhakika ili kuwasaidia katika kufanya kazi za ukaguzi na ufuatiliaji wa wafanayakazi katika maeneo yote ya kazi.

(c) Kamati inapendekeza kwa Serikali kuwapatia eneo Wizara ya Afya kwa upande wa Pemba kujenga Ofisi za Kudumu za Kitengo cha Afya Kazini kwani wamejistiri kwenye stoo na inapoteza hadhi na haiba kwa wageni wetu wanaofika kupata huduma hizo hali inayopelekea wengine kuamua kwenda vituo vya binafsi na kupelekea chanzo hiki kukosa mapato.

(d) Kamati pia inazishauri Wizara nyengine za Serikali pamoja na taasisi zake kufanya kazi kwa mashirikiano makubwa na kitengo hiki ili kuepusha maadhara yanayoweza kujitokeza hasa katika usalama wa wafanyakzi na fidia za ajali kazini.

(e) Kamati inaishauri Serikali kupitia Bohari Kuu ya Dawa na Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali kukiunganisha Kitengo hiki katika mfumo wa mgao wa vifaa na vitendanishi ili kuepusha kukosekana kwa baadhi ya vifaa na vitendanishi katika maabara hivyo kuwalazimu wateja kwenda hospitali binafsi.

## 3.5 PROGRAMU KUU YA HUDUMA ZA TIBA

Programu Kuu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo mbili (2) ikiwemo Programu Ndogo ya Huduma za Uchunguzi pamoja na Programu Ndogo ya Huduma za Matibabu ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imekadiriwa kutumia Tanzania Shilingi Bilioni Tisini, Milioni Mia Nne na Tisini, Laki

Sita na Ishirini na Sita (90,490,626,000/=) kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa malengo ya programu hii. Aidha, dhumuni kuu la kuanzishwa kwa programu hii ni kusimamia utoaji wa huduma bora za afya kwa Hospitali za Wilaya na Mikoa pamoja na kusimamia Taasisi mbali mbali za Wizara zikiwemo Mpango wa Damu Salama, Hospitali Binafsi, Huduma za Uchunguzi, Baraza la Wauguzi na Wakunga, Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi, Bohari Kuu ya Dawa, Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Afisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, Baraza la Madaktari na Taasisi ya Utafiti wa Afya.

## A. BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR

Bohari Kuu ya Dawa ina jukumu la kupokea, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa vya utabibu, reajenti pamoja na vifaa vyengine vya uchunguzi kwenye hospitali na vituo vyote vya afya vya Serikali na baadhi ya vituo vya binafsi Unguja na Pemba. Vile vile, Kamati ilipata taarifa kwamba manunuzi ya dawa yanafanywa na Wizara kupitia Kitengo chake cha Manunuzi (PDMU) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI BOHARI KUU YA DAWA

(a) Uhaba wa Rasilimali watu ikiwemo wafamasia, fundi sanifu dawa, afisa TEHAMA, afisa manunuzi, mkaguzi wa ndani, mafundi, wahasibu, ‘biomedical engineer’ na wanasheria.

(b) Bajeti ndogo ya kuendeshea huduma ni changamoto kubwa kwa Bohari ya Dawa Pemba kwa ajili ya utoaji wa huduma za usambazaji wa dawa kwa ufanisi.

(c) Uhaba wa vitendeakazi (Forklift na pallet stackers) na kompyuta.

(d) Uchache wa leseni za 'mSupply' jambo linalopelekea ucheleweshaji wa huduma za usambazaji unaotokana na msongamano wa watumiaji.

(e) Kukosekana kwa ulinzi wa uhakika katika Bohari Kuu ya Dawa Pemba.

(f) Kiasi cha dawa kinachopokelewa hakikidhi mahitaji ya kuwahudumia wateja kulingana na mahitaji husika.

(g) Uletaji wa dawa za misaada katika Bohari bila ya taarifa kwa wakati.

(h) Uhaba wa mawasiliano baina ya Bohari Kuu ya Dawa, Afisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali, Kitengo cha Manunuzi na Wahasibu hali ambayo inakosesha ufanisi kwenye mnyororo wa ugavi.

(i) Uwepo wa mrundikano wa vifaa katika Bohari kutoka kwa wadau mbali mbali wanaokosa muongozo wa usambazaji wake.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuandaa utaratibu maalum kwa dawa zinazonunuliwa kwa ajili ya Hospitali na vituo vya Afya Pemba kupelekwa moja kwa moja Pemba ili kuepusha ucheleweshaji wa huduma kwa hospitali na vituo hivyo.

(b) Kamati inaishauri Serikali juu ya suala zima la upatikanaji wa leseni za 'mSupply' kuongezwa ili kwenda sambamba na mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu matumizi ya mfumo huo kwa Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika kazi zao.

(c) Kamati inaiomba Wizara ya Afya kufanya mazungumzo na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ juu ya suala zima la kupatiwa walinzi katika maeneo yao ya Bohari ili kuimarisha usalama wa mali za Serikali.

(d) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya kwamba misaada yote inayoletwa kutoka kwa Wahisani mbali mbali kwenda Bohari Kuu ya Dawa ifuate utaratibu uliopo chini ya Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ili kuepusha uingizwaji wa dawa zilizokuwa zimeshamaliza muda wa matumizi.

(e) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea bajeti Bohari ya Kuu ya Dawa kwa lengo la kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi ili kuondokana na uchelewaji wa uangizaji wa dawa nchini.

(f) Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Serikali Mtandao kurekebisha kasoro ndogo ndogo ambazo zinasababisha kuzorota kwa suala la urahisishaji wa usambazaji wa dawa kupitia Mtandao.

(g) Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu wa kuipatia Bohari ya Dawa ya Vitongoji wafanyakazi wa kutosha pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kufanya shughuli zao bila ya kutegemea watendaji kutoka Bohari Kuu ya Dawa Maruhubi.

## B. MFAMASIA MKUU WA SERIKALI

Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Dawa (National Medicine Policy), hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu, vifaa vya utibabu na utumiaji sahihi wa dawa (Rational Medicine Use). Katika kufikia lengo hilo Ofisi ya Mfamasia Mkuu ina dhamana ya kufanya tathmini ya mahitaji ya dawa muhimu pamoja na vifaa vya utabibu (Quantification), kuratibu dawa ununuzi wa dawa muhimu na vifaa vya utibabu, kufanya ukaguzi

(Supportive Supervition) katika Hospitali ya Vituo vya Afya, ili kuhakikisha utunzaji bora na utumiaji sahihi wa dawa pamoja na kuangalia mwenendo wa dawa na vifaa vya utabibu (Supply Chain) hadi kumfikia mtumiaji/mgonjwa, kusimamia matumizi sahihi ya dawa kama miongozo inavyoelekeza.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA MFAMASIA MKUU WA SERIKALI**

(a) Mgao mdogo wa fedha za matumizi mengineyo (OC) ambapo huisababishia Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa ufanisi.
(b) Kukosekana kwa huduma ya mtandao (internet) katika vituo vya afya, jambo hilo hupelekea ucheleweshaji wa kuwasilisha ripoti za mahitaji ya dawa kwa wakati (R&R).
(c) Ofisi ya Mfamasia Dhamana Pemba kutokuwa na usafiri kwa ajili ya kazi za Ofisi kama vile ukaguzi na kutembelea hospitali pamoja na vituo vya afya. Mara nyingi ofisi imekuwa ikiomba na kutumia gari ya Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya kufanya kazi zake, hata hivyo, kufuatia kuongezeka kwa kazi za usambazaji wa dawa kila mwezi gari hiyo imekuwa haipatikani.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea mgao wa fedha za matumizi mengineyo (OC)

Ofisi ya Mfamasia Mkuu ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa ufanisi na ubora kama walivyojipangia katika bajeti husika.

(b) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wakala wa Mkonga wa Mawasiliano(ZICTIA) kuimarisha huduma ya mtandao katika vituo vyote vya afya pamoja na hospitali kwa ajili ya kurahisisha utumaji wa taarifa muhimu za afya zikiwemo za matumizi na maombi ya dawa (R&R).

(c) Kamati inaiomba Serikali kuipatia gari Ofisi ya Mfamasia Dhamana Pemba ili iweze kufanya kazi zake za kila siku kwa lengo la kuongeza ufanisi katika mnyororo wa ugavi.

## C. TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) imeanzishwa kwa Sheria Namba. 5 ya Mwaka 2018. Taasisi hii ni miongoni mwa Taasisi muhimu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mujibu wa Sheria ya kuanzishwa kwake, Taasisi ya Utafiti wa Afya imepewa majukumu ya kusimamia upatikanaji wa taarifa za kisayansi kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha njia na mbinu mbali mbali za tiba na udhibiti wa magonjwa ya binaadamu nchini ili kufikia malengo yaliokusudiwa.

### CHANGAMOTO ZA TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)

(a) Taasisi hii inakabiliwa na changamoto mbali mbali kama vile fedha za kuendeshaa tafiti muhimu, fedha za kumalizia ujenzi wa majengo

yaliyokusudiwa kuwa maabara ya kuchunguzia wanyama, maabara ya 'Biochemistry'.

(b) Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa Mkurugenzi Mkuu pamoja na watendaji wa Taasisi hiyo.

(c) Kuchelewa kwa kukamilika kwa ujenzi wa maktaba na ukumbi wa kufanyia mikutano (Scientific Conferrence).

(d) Kutokufanyiwa malipo ya ununuzi wa samani za Ofisi (furnitures), ambapo jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Mbili Hamsini na Tisa, Laki Sita na Themanini (259,680,000/=) wanazodaiwa na "Darworth Manufactures" ambao ndio wasambazaji wa samani. Samani hizo zilipokelewa tangu mwezi wa Disemba, 2021 na barua ya kuomba kufanyika kwa malipo ilitoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwenda kwa Katibu Mtendaji Tume ya Mipango tangu tarehe 08/02/2022, lakini mpaka tunapokea taarifa ya Taasisi hii malipo hayo bado hayajafanyika. Aidha, Taasisi imepokea barua kutoka kwa wasambazaji kuhusu dhamira yao ya kuja kuchukua samani zao.

(e) Kuchelewa kujazwa kwa nafasi za Kurugenzi za Ndani za Taasisi hiyo hali iliyopelekea watu kukaimu nafasi hizo kwa muda wa miaka mitano tangu kuanzishwa kwa Taasisi hiyo mwaka 2018 ambapo ni kinyume na utaratibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2014.

(f) Changamoto ya matumizi ya Mfumo wa Manunuzi ulioanzishwa na Mamlaka ya Manunuzi ya Serikali (e-proz), hali inayopelekea watumishi kushindwa kufanya malipo ya manunuzi yoyote ya Serikali.

(g) Ukosefu wa maeneo kwa ajili ya kuanzisha shamba darasa la mimea ya tiba asili ambayo inahitajika kufanyiwa utafiti kwa ajili ya matumizi ya

binaadamu licha ya maombi ya kuwasilishwa kwenye Wizara husika na Kilimo.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikana na Wizara ya Afya kuliangalia upya suala la kukaimu nafasi za Kurugenzi za Ndani kwa muda mrefu kinyume na matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya Mwaka 2011, hali inayopelekea watendaji hao kukosa haki pamoja stahiki zao za kiutumishi.

(b) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwapatia fedha Taasisi ya Utafiti wa Afya kwa ajili ya kufanya malipo ya samani ambazo walizikopa kutoka kwa wasambazaji kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa Ofisi.

(c) Kamati inaishauri Serikali kuipatia usafiri wa uhakika Taasisi hii ili kuwasaidia watendaji pamoja na Mkurugenzi Mkuu kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi hasa ikizingatiwa Taasisi yao ikon je ya Mji.

(d) Kamati pia inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuipatia eneo maalum Taasisi hii kwa ajili ya kuanzisha Shamba Darasa la mimea ya tiba asili kwa ajili ya kuenzi mimea adimu inayotoweka duniani ambayo ni muhimu kwa tiba ya afya kwa binaadamu.

(e) Kamati inaishauri Mamlaka ya Manunuzi Serikalini kabla ya kuanzisha mfumo wowote kuwapatia mafunzo watendaji wote wanaohusika na matumizi ya mfumo huo kwa lengo la kupunguza changamoto za matumizi yake.

## 3.6PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI WA URATIBU WA WIZARA

Programu hii inahusika na usimamizi wa rasilimali watu, rasilimali fedha, manunuzi, sheria na shughuli nyengine za uendeshaji wa Wizara. Aidha, ina jukumu la kuandaa na kusimamia Sera, Miongozo, Mipango pamoja na Kuratibu taarifa za Afya.

### CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA AFYA

(a) Upungufu wa wafanyakazi wa kada mbali mbali za afya wakiwemo 'radiographers', 'anaesthetist', 'biomedical engineers', 'nurses', 'doctors' n.k.) pamoja na watendaji wengi wa hospitali kutokuwa na ujuzi wa kutosha kwenye taaluma zao na kupelekea baadhi ya huduma kutokidhi viwango.

(b) Kuharibika kwa mashine za uchunguzi mara kwa mara kutokana na matumizi makubwa yam ashine hizo.

(c) Uingiaji usioridhisha wa fedha za kuendeshaa hospitali na kupelekea huduma nyingi za hospitali kuzorota.

(d) Kuendelea kukosekana kwa baadhi ya vifaa tiba kama vile mashine ya 'arterial blood gases' na mashine ya kusafisha figo (Dialysis) ndani ya 'ICU'.

(e) Uchakavu wa baadhi ya vituo vya Afya vya Daraja la Kwanza ambapo kunapelekea baadhi ya huduma kutotolewa ipasavyo.

(f) Ukosefu wa miundombinu ya TEHAMA hasa kwenye vituo vya afya, hali inayopelekea kwa taarifa za afya kutokutumwa kwa wakati kwenye Mfumo wa DHIS2.

(g) Upungufu wa vifaa tiba, vitenganishi na baadhi ya dawa inayotokana na Wizara kutoingizwa fedha za kutosha za ununuzi wa dawa, vitenganishi pamoja na vifaa tiba.

(h) Kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha za ziada (variations) katika miradi yote inayotekelezwa kupitia fedha za UVIKO - 19 hali iliyopelekea Wizara kuwa na ongezeko la fedha la Bilioni Ishirini na Moja (21,000,000,000/=) mbali na fedha ya awali walizopatiwa Bilioni Themanini (80,000,000,000/=).

(i) Kupangiwa kiwango kikubwa cha makusanyo yatokanayo na vyanzo vya mapato ya ndani kinyume na hali halisi ya Wizara ilivyo ambapo katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Wizara ya Afya ilipangiwa kukusanya Shilingi Bilioni Ishirini na Tano za Kitanzania (25,000,000,000/=). Katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2022 Wizara ya Afya ilipangiwa kukusanya Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Sita na Thamanini na Sita, Laki Tano na Thelathini na Tatu Elfu za Kitanzania (9,686,139,533.33/=) kutoka katika vyanzo vya mapato vya Wizara, ambapo hadi kufikia Disemba imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne na Thelathini na Mbili, Laki Sita na Thamanini na Nane, Mia Sita na Sabini na Tisa za Kitanzania (432,688,679.10/=) sawa asilimia na 4.47.

(j) Ucheleweshwaji wa ukamilishaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba wa watumishi katika Hospitali ya Kivunge kwa Unguja na Hospitali ya Abdalla Mzee na Micheweni kwa Pemba.

(k) Kuchelewa kumalizika kwa baadhi ya Miradi ya Hospital za Wilaya ndani ya Wakati uliopangwa.

(l) Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa Hospital ya Wete.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaipongeza Wizara ya Afya kwa kufanya ukarabati wa Vituo vya Afya 11 vya Daraja la Kwanza na kukamilisha Ujenzi ya wa baadhi Hospitali 10 za Wilaya na 1 ya Mkoa nayo kuendelea na ujenzi kwa lengo la kutoa huduma bora na  za kisasa.

(b) Kamati inaipongeza tena Wizara ya Afya kwa kuweza kuandaa Kambi mbali mbali za Upasuaji ikiwemo Kambi ya Magoti na Nyonga kwa kushirikiana na Hospitali ya MOI ambapo wananchi zaidi ya 30 walifaidika na huduma hizo zilizotolewa kwa mara ya kwanza hapa Zanzibar.

(c) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa Wizara husika wakati wa kupanga mafungu ya Mapato ya Wizara pamoja na Taasisi zake zote zinazokusanya kupitia vyanzo vyake vya ndani ili kukadiria bajeti yenye uhalisia kwa mwaka husika na sio bajeti ya kufikirika.

(d) Kamati inaishauri Serikali inapotekeleza Miradi mikubwa ya Maendeleo kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wa Wizara husika ili kuepusha changamoto ya matumizi ya ziada ya fedha za Serikali kwa kuwepo ongezeko la kazi za ziada nje ya mikataba ya awali na Wakandarasi.

(e) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuweka miundombinu ya TEHAMA kwenye Vituo vyote vya Afya kwa Unguja na Pemba ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za wagonjwa wanafika kwa ajili kuhudumiwa katika vituo hivyo.

(f) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaingizia fedha kwa wakati Wizara ya Afya kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yao kama walivyojipangia

kwenye bajeti, kwani kuchelewa kupatikana kwa fedha hizo kunasababisha kuzorota kwa shughuli nyingi za uendeshaji wa hospitali pamoja na vituo vya afya.

(g) Kamati inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kuharakisha upatikanaji wa kibali cha uajiri wa wafanyakazi wapya wa kada mbali mbali za afya wakiwemo ‘radiographers’, ‘anaesthetist’, ‘biomedical engineers’, ‘nurses’, ‘doctors’ ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa wataalamu na madaktari katika hospitali zetu.

(h) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuandaa mpango Madhubuti wa kuwasomesha na kuwaendeleza madaktari na wauguzi waliopo katika hospitali zetu wakiwemo ‘cardiothoracic’, ‘surgery’, ‘anaesthesia’, ‘urology’, ‘paediatric surgery’, ‘ophthalmology’, ‘radiation oncologist’, ‘surgical oncologist’, ‘neurosurgery’, ‘gastroenterology’, ‘emergency medicine’, ‘intensivist’, ‘vascular surgery’, ‘maxillofacial surgery’, ‘neurologists’, ‘haematologists’, ‘reconstructive surgery’ kwa lengo kuwaongezea ujuzi katika kazi zao za kila siku.

(i) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiwezesha Hospitali ya Mnazi Mmoja kuagiza na kununua dawa kupitia Kitengo chake cha Manunuzi moja kwa moja badala ya kupitia Bohari Kuu ya Dawa kwa ajili ya kurahisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa wakati wote.

(j) Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la ucheleweshwaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za watumishi katika Hospitali ya Kivunge kwa Unguja na Hospitali ya Abdalla Mzee na Micheweni kwa Pemba ili kuwaondoshea usumbufu watumishi wanaofanya kazi kwenye hospitali hizo ambao wanaishi mbali na vitio vyao vya kazi.

(k) Kamati inaishauri Serikali kuwasiliana na Wafadhili wa ujenzi wa Hospitali ya Wete ili Hospitali hiyo ijengwe kwa mujibu wa Makubaliano.

## 4. WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni miongoni mwa Wizara 18 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Awamu hii ya Nane. Wizara hii inatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia mpangilio wa Programu Kuu Tatu na Programu Ndogo Tano katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Programu zenyewe ni hizi zifuatazo:

(a) Programu Kuu ya Hifadhi ya Jamii;
(b) Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji;
(c) Programu Kuu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia.

Wizara hii imeundwa na Idara nne (4) na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

(a) Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
(b) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
(c) Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;
(d) Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee; na
(e) Ofisi Kuu Pemba.

Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hizo, Kamati ilifanya ziara katika Idara na sehemu mbali mbali kwa lengo la kuona mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Programu zilizopangwa pamoja na kubaini changamoto tofauti zinazokwamisha utekelezaji wa shughuli katika sehemu hizo na kuziwasilisha Serikalini kwa njia ya ushauri na kutafuta namna bora itakayoweza kutumika katika kuzipatia ufumbuzi wa kudumu changamoto

hizo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Aidha, utekelezaji wa shughuli za Wizara unasimamiwa na miongozo na mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambayo inatoa miongozo katika kukuza Ustawi wa Jamii kwa watu wote kwa kuimarisha upatikanaji na utoaji huduma bora na endelevu zinazozingatia Jinsia, Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Ulinzi na Hifadhi ya Mtoto pamoja na kuwawezesha wanajamii masikini na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

Wizara inaendelea kusimamia na kutekeleza Malengo ya Dira ya 2050 ya Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 – 2025, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021-2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030) na Kusimamia Sera ya Jinsia ya Zanzibar 2016, Sera ya Hifadhi ya Jamii 2014, Sera ya Hifadhi ya Maendeleo ya Mtoto 2002, Sheria ya Mtoto, Nam. 6 ya mwaka 2011 na Sheria ya Wazee Nam. 2 ya mwaka 2020.

## 4.1PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII

Programu Kuu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo moja ya Hifadhi ya Jamii ambapo shughuli zinazotekelezwa ni kuzingatia mikakati ya Kitaifa na Kimataifa, Sheria ya Mtoto, Nam. 6 ya mwaka 2011, Sheria ya Fidia, Nam. 15 ya mwaka 1986 na mabadiliko yake Sheria Nam. 5 ya mwaka 2005, Sheria ya Wazee, Nam. 2 ya mwaka 2020 na Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa programu hii ni kutoa huduma kwa wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, kusimamia na kutekeleza Mpango wa Pencheni Jamii na Kuimarisha Uratibu wa Hifadhi ya Jamii na Hifadhi ya Mtoto, ambapo jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Mia Nne na Arubaini na Mbili, Laki Tano na Hamsini na Tano (13,442,555,000/=) zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

**KITENGO CHA PENCHENI JAMII**

Pencheni Jamii inaratibiwa chini ya Programu Ndogo ya SQ010301 ya Uratibu wa Huduma ya Hifadhi ya Jamii, ambayo inatekeleza na Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee ambayo ina jumuku la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yanayoishi katika mazingira magumu.

Mpango wa Pencheni Jamii unaratibiwa na Kitengo cha Pencheni Jamii, ambapo kazi zake za kila siku ni pamoja na kuhakikisha wazee wanapatiwa Pencheni zao za kila mwezi, kuingiza wazee wapya na kutoa wazee waliofariki, kufanya uhakiki kwa ajili ya kuhakikisha vigezo vya wazee vimefikiwa kabla ya kuingizwa kwenye mpango, kujiridhisha na uwepo wa walengwa wanaonufaika na mpango huo na kufuatilia iwapo fedha za Serikali zinawafikia walengwa waliokusudiwa.

## CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KITENGO CHA PENCHENI JAMII

(a) Mfumo wa malipo ya wazee unakabiliwa na changamoto ya kiusalama na kiutendaji.

(b) Mazingira magumu ya uhakiki maalum wa wazee wa kuwafuata nyumba hadi nyumba hasa katika maeneo ya nje ya mji, kutokana na makaazi yaokutawanyika katika sehemu mbali mbali.

(c) Uhaba wa vitendea kazi ikiwemo kompyuta, makabati ya kuhifadhia kumbukumbu na ving'amuzi.

(d) Kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika katika ufuatiliaji wa kazi za Kitengo.

(e) Kukosekana internet kwa ajili ya kuingiza taarifa za walengwa katika mfumo

(f) Uhaba wa rasilimali watu katika Kitengo cha Pencheni Jamii.

(g) Wazee wengi kutokuwa na vitambulisho na baadhi vitambulisho vyao vimekuwa vikionesha umri mdogo.

(h) Kutumika vibaya Vibali vya Ruhusa (Power of Attorney) kwa watu wanaowawakilisha wazee wao wasiojiweza na wenye mazingira magumu.

(i) Baadhi ya wanufaika wa Pencheni Jamii hawafikii umri stahiki wa miaka 70 na wengine waliofikia umri 70 bado hawanufaiki, kutokana na kutokuwepo kwa nyaraka za uthibitisho kwa wazee hasa Vijijini.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Kitengo cha Pencheni Jamii kuwafanyia uhakiki wazee wanaonufaika na Pencheni Jamii kila baada ya kipindi cha miezi mitatu, kwa ajili ya kuweza kuwatambua wanufaika hai wa pencheni hiyo.

(b) Kamati inaishauri kufuatilia na kuhakiki Vibali vya Ruhusa (Power of Attorney) vyote kwa watu ambao wanaopokea Pencheni Jamii kwa niaba ya wazee wao ili kuokoa fedha za Serikali Pamoja na kuepusha udanganyifu wa matumizi wa vibali hivyo.

(c) Kamati inaishauri jamii kuongeza mashirikiano na masheha, watendaji wa Wizara pamoja na Viongozi wengine katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwenye mambo ya Pencheni Jamii.

(d) Kamati inaishauri Wizara kuendelea na programu mbali mbali za kuelimisha jamii kuhusu masuala ya Pencheni Jamii kupitia vyombo vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, Instagram na YouTube.

(e) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la upatikanaji wa vitambulisho vya Wazee waliofikia umri wa kupokea Pencheni hiyo.

(f) Kamati inapendekeza kwa Serikali kulipa kipaumbele katika mipango yake ya ujenzi wa majengo ya Serikali, upatikanaji wa Ofisi ya kudumu ya Kitengo cha Pencheni Jamii, kwani walipo sasa mazingira yake si rafiki na utendaji wa kazi zao.

## 4.2PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA

Kimsingi Programu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Jinsia na Watoto ambapo dhumuni kuu ni kuwajengea uwezo na watoto ushiriki katika Mabaraza ya Watoto, kusimamia na kuendeleza juhudi za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto na kusimamia shughuli za maendeleo ya jamii. Takribani jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tatu na Hamsini na Nane, Laki Moja Elfu Hamsini na Nne (1,358,154,000/=) zimetengwa kwa mwaka fedha 2022/2023.

### A. WARATIBU WA SHEHIA YA MJINI MAGHARIBI

Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni moja kati ya idara yenye jukumu la kusimamia masuala yanayohusiana na Maendeleo ya Wanawake na Watoto dhidi ya masuala ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia yanayowakumba wanawake na watoto katika jamii yetu.

Aidha, Idara hii imeundwa ikiwa na Divisheni kuu nne ambazo ni Divisheni ya Maendeleo ya Jamii, Divisheni ya Jinsia, Divisheni ya Maendeleo ya Watoto na Divisheni ya Uratibu wa Mapambano ya Kupinga Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, ambapo kupitia Divisheni hizo Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina majukumu yafuatayo:

(a) u

ratibu na kusimamia utekelezaji wa haki, ulinzi na maendeleo ya

wanawake na watoto;

(b) kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Programu zinazohusumaendeleo ya Wanawake na Watoto;

(c) kuhamasisha jamii (Wanawake na Wanaume) kuzingatia usawa wa kijinsia;

(d) kuratibu mapambano dhidi ya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto;

(e) kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika kulindana kuendeleza haki za Wanawake na Watoto;

(f) katika kuhakikisha kuwa uratibu wa shughuli za mapambano ya kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, Idara ina jukumu la kuwawezesha waratibu wa wanawake na watoto katika shehia ili kufanya shughuli zao kwa ufanisi za kuibua na kufuatilia vitendo vya kupambana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika shehia zao.

**CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WARATIBU WA SHEHIA YA MJINI MAGHARIBI**

(a) Waratibu wa wanawake na watoto wa shehia kuwekewa vitisho wakati wa ufuatiliaji wa matukio ya udhalilishaji katika jamii na taasisi za kisheria.

(b) Kutokuwepo kwa mashirikiano ya kutosha kati ya Waratibu, Mabaraza ya Watoto na baadhi ya Masheha.

(c) Ongezeko la vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na Watoto hasa Mkoa wa Mjini Magharibi.

(d) Dhana potofu juu ya uendeshaji na usimamizi wa mabaraza ya watoto

ngazi ya shehia.

(e) Muhali katika utoaji wa ushahidi Mahakamani.

(f) Kuvunjika kwa ndoa hali inayopelekea kutelekezwaji wa wanawake na watoto.

(g) Uelewa mdogo kwa baadhi ya wazazi kuhusu kuripoti kesi za masuala ya udhalilishaji na ukatili wa wanawake na watoto.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kutoa taaluma kwa jamii kuhusu masuala ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto kuhusiana na kujitambua, kuwa jasiri, kuacha muhali pamoja na kukataa kudhalilishwa.

(b) Kamati inapendekeza kuangaliwa kwa kina na kutumika mbinu mbadala katika kushughulikia masuala ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto ili kuweza kupunguza na hatimae kumaliza kabisa vitendo vya ukatili na udhalilishaji katika jamii yetu.

(c) Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kutenga bajeti maalum kwa ajili ya Waratibu wa Shehia ili kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi.

(d) Kamati inaishauri Serikali kurejesha Polisi Jamii katika shehia zote za Unguja na Pemba kwa lengo la kuweza kukinga pamoja na kudhibiti vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto katika maeneo yetu.

(e) Kamati inashauri kuwepo kwa mashirikiano mazuri miongoni mwa Waratibu wa Shehia, Masheha, Mabaraza ya Watoto ya Shehia,

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Jeshi la Polisi, Waendesha Mashtaka, Vituo vya Mkono kwa Mkono pamoja na jamii kwa jumla kwa lengo la kuvitokomeza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto katika nchi yetu.

## B. MASUALA YA UKATILI NA VITENDO VYA UDHALILISHAJI KWA WANAWAKE NA WATOTO ZANZIBAR

Masuala ya Ukatili na Vitendo vya Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto vimekuwa vikiendelea kutokea katika jamii yetu ya Zanzibar licha ya juhudi kubwa zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kuzuia, kulinda pamoja na kupambana na vitendo hivyo siku hadi siku.

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza kazi zake za kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa Wizara inazozisimamia ikiwemo na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilipata nafasi ya kukutana na Waratibu wa Shehia wanaoshughulikia Masuala ya Ukatili na Udhalilishaji Wanawake na Watoto, Vituo vya Mkono kwa Mkono vya Wilaya tofauti za Unguja na Pemba kwa lengo kufahamu hali halisi ya tatizo, changamoto pamoja na kutafuta namna bora ya kutatua janga hilo.

**CHANGAMOTO ZA MASUALA YA UKATILI NA VITENDO VYA UDHALILISHAJI KWA WANAWAKE NA WATOTO ZANZIBAR**

(a) Muhali wakati kutoa ushahidi kuhusiana na kesi zinazohusiana na Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto unasababisha ucheleweshwaji wa usikilizwaji wa kesi hizo katika vyombo vya kisheria na baadhi ya wakati kufutwa kwa kesi hizo.

(b) Waratibu wa Shehia kukosa mashirikiano kutoka katika jamii wakati wa kushughulikia masuala yanayohusiana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji Wanawake na Watoto hali inayopelekea waratibu hao kukosa ari ya kuendelea kufuatilia kesi hizo.

(c) Watoto kushiriki kwenye shughuli za kuokota karafuu maarufu (Mpeta) husababisha baadhi ya watoto kufanyiwa vitendo vya Udhalilishaji.

(d) Rushwa kwa baadhi ya watendaji wa Taasisi zinazoshughulikia masuala ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji Wanawake na Watoto hali inayopelekea baadhi ya kesi kukosa muendelezo wake na hatimae kufutwa kinyume na utaratibu.

(e) Kutokuwepo kwa usafiri wa pamoja kwa ajili ya kuwashughulikia wahanga katika vyombo vya sheria baada ya tukio kutokea linalohusiana na masuala ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto na mwisho kupelekea kupotea kwa ushahidi.

(f) Kukosekana kwa malezi ya pamoja katika jamii ambapo tafiti nyingi zinaonesha watoto wengi wanaokabiliwa na changamoto hii ya udhalilishaji wanakosa malezi ya pamoja katika familia zao kutokana na wazee wao kutengana.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inapendekeza kwa Taasisi za Serikali na Binafsi pamoja na jamii kwa ujumla kuongeza mashirikiano katika kukinga pamoja na kupiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto vilivyoshamiri katika jamii kwani mashirikiano ya pamoja ndio yatakayoondoa kabisa vitendo hivyo katika jamii zetu *"Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu"*.

(b) Kamati inaishauri Wizara kuweka mazingira rafiki kwa wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wakati wa kushughulikia kesi zao.

(c) Kamati pia inaendelea kupendekeza kuwepo kwa utaratibu wa utoaji wa elimu ya ndoa kabla na baada kufunga ndoa kwa wanandoa kwa lengo la kufahamu majukumu ya mume na mke katika ndoa ikiwemo suala la kuwapatia haki za msingi watoto ambazo ni chakula, elimu, makaazi, mavazi ili kuweza kuwalinda pamoja na kuwakinga na vitendo vya ukatili na udhalilishaji watoto na jamii kwa ujumla ili kusaidia kupunguza na hatimae kutokomeza janga hilo.

(d) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Taasisi nyengine za Serikali na Binafsi kuvijengea uwezo Vituo vya Mkono kwa Mkono, na Taasisi nyengine zinazohusika na vitendo vya Udhalilishaji ili kuweza kuyashughulikia masuala hayo yanapofikishwa katika maeneo yao ya kazi.

(e) Kamati inaishauri jamii kuripoti vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto mara tu baada ya kutokea vitendo hivyo na kupeleka taarifa katika sehemu husika ikiwemo Waratibu wa Shehia,

Vituo vya Mkono kwa Mkono, Maafisa wa Ustawi wa Jamii na Polisi kwa ajili ya kuweza kushughulikiwa kwa haraka na wakati ili kuwepo kwa ushahidi.

(f) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupiga marufuku kwa wanafunzi wa waliochini ya umri wa miaka kumi na nane (18) kufanya kazi za uchumaji, uokotaji na uanikaji wa karafuu (Mpeta), kwani Kamati imebaini kwamba kipindi cha harakati hizo ongezeko la idadi ya kesi zinazotokana na vitendo vya udhalilishaji.

## 4.3PROGRAMU KUU YA UTAWALA UENDESHAJI WA WIZARA

Kazi kuu za Programu hii zinatekelezwa kupitia Programu Ndogo Tatu ambazo ni Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji, Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu Kuu hii ilipangiwa kutumia jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Thelathini na Tano, Laki Nne na Tisini na Moja (1,135,491,000/=) kwa ajili ya kutoa huduma za Utawala wa Uendeshaji, Kusimamia Sera na Miongozo pamoja na Kuratibu na Kutekeleza Shughuli za Wizara Pemba.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

(a) Kuwepo kwa bajeti ambayo haikidhi mahitaji halisi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara imeshindwa kutekeleza majukumu

yake ya msingi waliopangiwa kwenye bajeti na kufanya uhaulishaji kwa baadhi ya vifungu vilivyomo ndani ya Wizara ili kutekeleza shughuli muhimu za Wizara.

(b) Kutokuwepo kwa mifumo imara ya kuhifadhi taarifa, hali inayopelekea kutokuwepo kwa taarifa sahihi kwa wazee wanaostahiki kupatiwa Pencheni Jamii na watoto wanaopata matatizo ya masuala ya ukatili na vitendo vya udhalilishaji.

(c) Ucheleweshaji wa upatikanaji wa Vitambulisho vya Pencheni Jamii kwa Wazee, hali inayopelekea Serikali kupoteza fedha nyingi kwa kuwalipa watu wasiostahiki.

(d) Gharama kubwa ya ulipaji wa kodi ya jengo ambalo linatumiwa na Wizara ambapo kwa mwaka kugharimuTanzania Shilingi Milioni Sitini (60,000,000/=).

(e) Upungufu wa vitendeakazi vya ofisi hali inayopelekea kupungua ufanisi wa utekelezaji wa kazi za Wizara.

(f) Uhaba wa rasilimali watu pamoja kuwepo kwa muitiko mdogo katika jamii katika suala zima la kutoa Ushahidi kwenye kesi za ukatili na vitendo vya udhalilishaji.

(g) Ukosefu wa usafiri kwa Wakurugenzi wa Wizara hivyo kulazimika kutumia gari ya Katibu ambayo ni chakavu kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya Wizara.

(h) Kuchelewa kupatikana kwa posho kwa Waratibu wa Shehia wanaofualitia Masuala ya Ukatili na Vitendo vya Udhalilishaji ambako kunapelekea kuwapunguzia ari ya utendaji kazi kwa Waratibu hao. Kwa mwaka 2022/2023 Wizara ilitumia fedha zake za matumizi mengineyo (OC) kwa ajili ya kuwalipa posho Waratibu hao.

(i) Kutokuwepo kwa Rasilimali watu na vifaa katika Ofisi ya Pemba, hali inayopelekea kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Aidha, Ofisi ya Pemba haina mtumishi wa masjala, hakuna sekretari na vifaa kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

(j) Ongezeko la idadi ya kesi za udhalilishaji na ukatili wa kijinsia na ucheleweshaji wa kusikiliza kesi hali inayopelekea wananchi kupoteza imani na Taasisi zinazoshughulikia kesi hizo.

(k) Kutokuwepo kwa taarifa sahihi za wazee wanaostahiki kupokea Pencheni Jamii kwa baadhi ya Shehia kwa Unguja na Pemba.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kulisimamia kwa karibu suala la upatikanaji wa vitambulisho vya Wazee wanaopokea Pencheni Jamii kwa ajili ya kuokoa fedha za Serikali pamoja na kudhibiti vitendo vya udanganyifu kwa baadhi ya wananchi wanaopokea pencheni hizo kwa niaba ya wazee wao.

(b) Kamati inashauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara kufanya kikao cha pamoja na masheha katika kulitafutia ufumbuzi suala zima la udanganyifu kwa baadhi ya wananchi ambao hawajafikia umri wa kupokea Pencheni Jamii.

(c) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwapatia eneo la ujenzi wa jengo la Wizara ili kuondokana na changamoto ya kukodi majengo kwa gharama kubwa.

(d) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwapatia magari Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,

Wazee na Watoto pamoja na kuwaingizia fedha za kununua vifaa vya ofisi.

(e) Kamati inapendekeza kwa Serikali kuandaa mfumo maalum wa uhifadhi wa taarifa za wapokeaji wa Pencheni Jamii pamoja na kesi za udhalilishaji na vitendo vya ukatili wa kijinsia ili kuwa na takwimu sahihi.

(f) Kamati inaishauri Wizara kuwaongezea posho Waratibu wa Shehia wanaoshughulikia masuala ya kesi za udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kila hali inaporuhusu kwani wanafanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi.

(g) Kamati inapendekeza kwa Serikali kuanzisha Kituo Jumuishi(One Stop Center) kitakachojumuisha taasisi zote zinazohusika na ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji katika kila Wilaya ili kupunguza udanganyifu, upotevu wa ushahidi na ucheleweshaji wa ushughulikiaji wa kesi hizo.

## 5. WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inaundwa na Sekta Nne ambazo ni:

*(i)* Sekta ya Habari;
*(ii)* Sekta ya Vijana;
*(iii)* Sekta ya Utamaduni; na
*(iv)* Sekta ya Michezo.

Sekta hizo zimeundwa na Idara, Mabaraza, Mashirika, Tume, Kampuni, Wakala na Afisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:

### 5.1SEKTA YA HABARI

*(a)* Idara ya Habari na Maelezo;
*(b)* Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*);
*(c)* Tume ya Utangazaji Zanzibar;
*(d)* Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (*ZGPA*);
*(e)* Kampuni ya Kuunganisha na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (*ZMUX*);
*(f)* Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar.

### 5.2SEKTA YA VIJANA

*(i)* Idara ya Maendeleo ya Vijana;
*(ii)* Baraza la Vijana Zanzibar.

## 5.3SEKTA YA UTAMADUNI

*(i)* Idara ya Utamaduni;
*(ii)* Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni;
*(iii)* Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar (*COSOZA*);
*(iv)* Baraza la Kiswahili (BAKIZA).

## 5.4SEKTA YA MICHEZO

*(i)* Idara ya Michezo;
*(ii)* Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ);
*(iii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
*(iv)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji
*(v)* Afisi Kuu Pemba.

## 5.5PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

Programu hii inaundwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji. Shughuli kuu zinazotolewa ni Urushaji wa Vipindi na Matangazo, kupitia TV na Redio, Utoaji wa Taarifa, Picha, Makala, Filamu na Sinema, Utoaji wa Magazeti, Usambazaji wa Maudhui, Kudhibiti na Kusimamia Shughuli za Utangazaji kupitia Sera na Sheria za Habari na Utangazaji, Kusimamia Shughuli za Uchapaji pamoja na kudhibiti na kusimamia shughuli za Vituo vya Utangazaji kupitia Sera na Sheria za Utangazaji ambapo jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Ishirini na Mbili, Milioni Mia

Tisa na Themanini, Elfu Sitini na Moja (22,980,061,000/=) zimepangwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

## A. KITUO CHA ZBC DAR-ES-SALAAM

Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam kimeanzishwa mwaka 2009 na kimekuwa tegemeo la habari kwa upande wa Tanzania Bara. Aidha, lengo kuu la kuanzishwa kwake ni kufanikisha usambazaji wa habari, kuandaa vipindi na kurusha hewani habari za matukio muhimu yanayotokea kwa upande wa Tanzania Bara zikiwemo habari za kisiasa, uchumi, utamaduni, michezo na kijamii.

Kuwepo kwake ni kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania na dunia kwa ujumla wanapata habari na matukio hayo kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia ZBC Televisheni na Redio.

### CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI KITUO CHA ZBC DAR-ES-SALAAM

(a) Uhaba na uchakavu wa vitendeakazi, vikiwemo kamera, gari na samani za Ofisi hali inayodhorotesha na kurudisha nyuma ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

(b) Uhaba wa baadhi ya wataalamu wakiwemo mhariri picha (video editor), fundi na uwepo wa dereva mmoja. Tokea kuanzishwa kwake, kituo kimekuwa hakina mtaalamu wa masuala ya uhariri picha na fundi ambaye ana weledi wa kuwezesha kufanikisha kazi kwa wakati.

(c) Ofisi haina nafasi ya kutosha hivyo kunapelekea usumbufu katika kufanikisha baadhi ya majukumu ya kazi. Studio ambayo inatumika kurekodi vipindi na kuandaa Taarifa ya Habari ni ndogo mno na haina viwango vinavyohitajika hali inayowakwaza kufanya ubunifu.

(d) Kuwepo kwa muundo ambao hadi sasa hautambui uwepo wa nafasi ya Mkurugenzi wa Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam hali inayopelekea kukosa haki zake za msingi pamoja na stahiki zake nyengine zilizopo kwa mujibu wa Sheria.

(e) Sheria ya ZBC Nam. 4 ya Mwaka 2013 ni ya muda mrefu na ina mapungufu mengi katika utekelezaji wake.

(f) Kutokuwepo kwa Kanuni ya Sheria ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC), Nam. 4 ya mwaka 2013, hali inayosababisha utekelezaji mgumu wa baadhi ya majukumu yao ya kila siku.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikali kulikamilisha kwa hatua zilizobakia suala la marekebisho ya mapendekezo ya Muundo mpya wa Shirika la Utangazaji Zanzibar ili kuweza kutambua baadhi ya nafasi ambazo katika Sheria ya Shirika hazikuwepo. Mfano halisi, nafasi ya Mkurugenzi Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam.

(b) Kamati inapendekeza tena kwa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kulishughulikia suala la ukosefu wa jengo la kudumu kwa Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam kwani kutokufanya hivyo ni kubakia kuazima ofisi.

(c) Kamati inaishauri Wizara kulipa kipaumbele suala la upatikanaji wa mtaalamu wa uhariri picha katika Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam ili kituo hicho kiweze kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi ya tansia ya habari.

(d) Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Bodi ya Shirika la Utangazaji Zanzibar wakati kwa kuajiri watendaji wapya wa Shirika kuzingatia upatikanaji wa dereva wa kudumu kwa Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam ili kuondoa changamoto iliopo sasa ya kuwepo dereva mmoja.

(e) Kamati inaishauri Wuzara kuifanyia marekebisho Sheria ya Shirika la Utangazaji ili kwenda sambamba na madhumuni ya kutungwa Sheria hiyo.

(f) Kamti inaishauri Wizara kutunga Kanuni ya Sheria ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) Nam. 4 ya mwaka 2013 kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Shirika hilo kwa ufanisi zaidi.

## B. TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR

Tume ya Utangazaji Zanzibar imeanzishwa chini ya Sheria Nam. 7 ya mwaka 1997 na miongoni mwa majukumu yake ni pamoja na kusajili na kutoa leseni kwa Vituo vya Utangazaji vya Redio, Televisheni na Mitandao ya Kijamii hapa Zanzibar.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TUME YA UTANGAZAJI

(a) Uhaba wa Rasilimali watu na uchakavu wa vitendeakazi vya Ofisi hali inayopelekea Tume kushindwa kutekeleza baadhi ya kazi zake kwa ufanisi na kusababisha kutofikia malengo waliyojipangia.

(b) Tume ya Utangazaji inakusanya mapato makubwa yanayoingia Mfuko Mkuu wa Hazina lakini Tume inashindwa kutumia sehemu ya mapato hayo.

(c) Vituo kushindwa kulipa ada kwa wakati hali ambayo inaipelekea Tume kutokukusanya mapato yake kama ilivyojipangia.

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

(a) Kamati inaipongeza Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kupitia Tume ya Utangazaji Zanzibar kwa ukusanyaji mzuri wa mapato unaotokana na vianzio mbali mbali vya ndani ikiwemo Ada ya Leseni, Ada ya Maombi ya Leseni na Ada ya Mwaka ya Leseni.

(b) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la upatikanaji wa jengo la kudumu la Ofisi ya Tume ya Utangazaji Zanzibar kwa ajili ya kuendesha shughuli zao ili kuepukana na gharama zisizo za lazima za kukodi jengo pamoja na gharama zinazotumika katika ununuzi wa vifaa na uwekaji wa mitambo inayotumika maeneo hayo waliyokodi.

(c) Kamati inaiomba Serikali kupitia na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiruhusu pamoja na kuiandalia Tume ya

Utangazaji mpango wa matumizi ya kiasi cha fedha wanazozikusanya (Retention) kupitia vyanzo vyao mbali mbali ili kuweza kuisaidia Tume ya Utangazaji katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

(d) Kamati inaishauri Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini pindi zinapotangazwa nafasi za ajira kuajiriwa kwa wataalamu wanaohusiana na Tasnia ya Habari na Mawasiliano ya Umma kwa ajili ya kutatua changamoto wanazokumbana nazo juu ya suala zima la uhaba wa wataalamu ili Tume iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

## C. KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI WA MAUDHUI ZANZIBAR (ZMUX)

Kampuni ua Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX) ni Kampuni ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni, Nam. 15 ya Mwaka 2013 na baadae kufanyiwa mapitio Mwaka 2018. Kampuni hii ni miongoni mwa Taasisi sita (6) zinazounda Sekta ya Habari na inatekeleza majukumu yake chini ya Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji. Majukumu makuu ya Kampuni hii ya Uuunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX) ni pamoja na kuanzisha na kuendeleza biashara ya maudhui katika mfumo wa dijitali, kuendleza miundombinu ya upokeaji na usambazaji wa maudhui (content), kuendeleza na kuimarisha huduma za utangazaji za ndani na nje ya nchi.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KAMPUNI YA USAMBAZAJI WA MAUDHUI (ZMUX)**

(a) Uchakavu wa vifaa unapelekea kukosekana kwa ubora wa kazi ikiwemo kukatikakatika kwa picha au kuganda kwa picha au sauti.
(b) Muundo wa Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) haukuzingatia stahiki za wafanyakazi.
(c) Uhaba wa vitendea kazi hali inayosababisha ZMUX kutofikia malengo waliojipangia kwa wakati.
(d) Posho za Mazingira hatarishi zimefutwa licha ya watendaji kufanya kazi ngumu na nyeti na hatarishi.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaipongeza Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui (ZMUX) kwa kupata uongozi ikiwemo Mkurugenzi wa ZMUX pamoja na Bodi.
(b) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulishughulikia suala la Muundo wa ZMUX na kukamilika kwa haraka, kwa lengo la kuiwezesha Kampuni hii kufanya kazi zake kwa mujibu wa matakwa ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma katika kusimamia haki na wajibu wa watendaji wao.
(c) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea bajeti Kampuni ya Usambazaji wa Maudhui, ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

(d) Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi suala la Posho la Mazingira Hatarishi kwa baadhi ya watendaji wa Taasisi za Serikali wakiwemo watendaji wa ZMUX kwa lengo la kuweza kufanya kazi kwa bidii kubwa, uzalendo na uadilifu.

## D. SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR (SMS)

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar limeanzishwa chini ya Sheria Nambari 11 ya mwaka 2008. Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) linachapisha magazeti manne (4) ambayo ni gazeti la siku (Zanzibar Leo, Magazeti ya kila wiki (Zanzibar Mail na Zanspoti) na gazeti la Zanzibar Leo Jumapili ambalo hutolewa kila siku Jumapili. Magazeti haya husambazwa Zanzibar nzima na Mikoa 22 ya Tanzania Bara kwa lengo la kusambaza taarifa zenye kuelimisha kuhusu mambo mbali mbali ya nchi, burudani na michezo.

### CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR (SMS)

(a) Kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu katika Shirika hali inayowasababishia kushindwa kufikia malengo waliojipangia ya makusanyo ya mapato. Baadhi ya madeni yameshakuwa ya muda mrefu tokea mwaka 2016 na hadi sasa taasisi hizo zinazodaiwa kushindwa kufanya marejesho yoyote ya malipo hayo. Hadi kufikia Disemba, 2022 Shirika linadai Tanzania Shilingi Milioni Mia Moja na Sabini na Tatu, Laki Tano na Sabini na Sita, Mia Mbili na Hamsini (173,576,250/=) kati ya fedha hizo Tanzania Shilingi Milioni Mia

Moja Ishirini na Tano, Laki Saba na Arubaini na Sita, Mia Mbili na Hamsini (125,746,250/=) zinadaiwa taasisi za Serikali na Binafsi Zanzibar na Tanzania Shilingi Milioni Arubaini na Saba, Laki Nane na Thelathini (47,830,000/=) kwa taasisi za Serikali na Binafsi ziliopo Tanzania Bara.

Aidha, jumla ya deni linalodai Shirika hadi kufikia Disemba, 2022 ni Tanzania Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Nane na Sitini na Tano, Laki Moja na Tisini na Sita na Tisini na Sita Elfu (2,865,196,096,000/=). Mchanganuo wa deni hilo ni kama unavyoonekana hapo chini:

| NAM. | DENI | JUMLA |
|---|---|---|
| 1. | Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | 2,310,448,896,000/= |
| 2. | Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | 554,747,200,000/= |
| | **JUMLA KUU** | **2,865,196,096,000/=** |

(b) Uchache wa matangazo ambapo Shirika lilikadiriwa kupokea na kuchapisha matangazo 450 kwa kipindi cha robo hii, hata hivyo, Shirika limeshindwa kufikia lengo na kupelekea kuchapisha matangazo 305 tu ambayo ni sawa na asilimia 66.

(c) Ushindani mkubwa wa biashara ya magazeti hivyo kupelekea mauzo hafifu ya magazeti.

(d) Kupanda kwa gharama za uchapishaji magazeti ambapo Shirika linatumia kiasi kikubwa cha mapato yake kugharamia uchapishaji.

(e) Kupata ruzuku ndogo ya OC ambayo Shirika inapokea kutoka Serikalini. Mfano halisi, kwa kipindi cha Oktoba – Disemba Shirika

lilipangiwa kupatiwa ruzuku ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Moja na Sabini (170,000,000/=) kwa ajili ya kusaidia uchapishaji wa magazeti fedha iliyopatikana hadi kufikia Disemba ni Tanzania Shilingi Milioni Thelathini na Sita (36,000,000/=) tu za utekelezaji wa kazi hiyo.

(f) Kupitwa na wakati kwa Sheria iliyoanzisha Shirika la Magazeti Zanzibar ambapo Kamati imebaini kuwa Sheria hiyo ina mapungufu mengi katika utekelezaji wake.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la Magazeti Zanzibar kusimamia maamuzi yaliotolewa na Serikali juu ya suala zima la ulipwaji wa deni kubwa la usambazwaji wa magazeti kwa taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Kamati inalishauri Shirika la Magazeti Zanzibar kuongeza usambazaji wa magazeti katika maeneo ya uingiaji wa wageni katika Viwanja vya Ndege pamoja na Bandari zetu zote ili kuongeza mapato ya makusanyo pamoja na kuitangaza nchi yetu.

(c) Kamati pia inaipongeza Wizara kupitia Shirika la Magazeti Zanzibar kwa kuweza kupanua na kuongeza wigo wa usambazaji wa magazeti Tanzania Baraza. Ambapo awali idadi ya Mikoa iliyokuwa ikifikiwa ni 11 na sasa magazeti yanasambazwa Mikoa 22. Vile vile, Shirika kwa kuweza kuongeza idadi wa Mawakala kutoka 14 hadi 36 na kuongeza idadi ya wauzaji wadogo kutoka 22 hadi 150.

(d) Kamati inapendekeza kwa Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuharakisha mapitio ya Sheria ya Shirika la Magazeti Zanzibar ili iweze kwenda na mahitaji ya soko la kibiashara la ushindani ndani na nje ya nchi pamoja na kufikia azma ya utekelezaji wa Serikali ya kuanzishwa kwa Shirika hilo.

(e) Pia, Kamati inaishauri Serikali kuandaa kikao cha pamoja kati ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuliangalia upya suala la uingizwaji mdogo wa fedha za ruzuku kwa Shirika la Magazeti kwani kubakia kama ilivyo ni kulirudisha nyuma Shirika kimakusanyo na kiutendaji katika soko la ushindani wa kibiashara na mwisho kulipelekea kurudi kuwa tengemezi.

## E. WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA)

Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA) umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 12 ya mwaka 2018. Majukumu makuu ya Wakala ni kutoa huduma za uchapaji pamoja na uuzaji wa vifaa vya ofisi na vya kuandikia kwa Taasisi za Serikali na Binafsi. Wakala wa Uchapaji unasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na anaawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Uchapaji.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA)**

(a) Uhaba wa mitambo hali inayopelekea baadhi ya mitambo kuharibika kutokana na kufanya kazi bila ya kupumzika.
(b) Baadhi ya wasambazaji wa nje ya Zanzibar hawataki kujisajili katika Mfumo wa Kielektroniki ulio chini ya Mamlaka ya Ununuzi hali inayowasababishia kushindwa kufanya manunuzi.
(c) Uhaba wa wafanyakazi hasa katika sehemu ya Kiwanda.
(d) Kutopatikana kwa fedha za Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Uchapaji ulioidhinishwa tokea mwaka wa fedha 2021/2022.
(e) Kutokuwa na Ghala la kudumu la kuhifadhia vifaa vya Bohari hali inayowapelekea kukodi maeneo kwa fedha nyingi.
(f) Kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu wanayodai Wakala wa Uchapaji kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Makampuni ya Binafsi baada ya kupatiwa kuduma mbali mbali zinazotolewa na Wakala.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Wizara kuisimamia Sheria pamoja na muongozo ulitolewa na Serikali la kuwataka Wizara pamoja na Taasisi zote za Serikali kupelekea kazi zake za uchapaji na za ununuzi wa vifaa vya Maafisi na kufundishia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kufanya kinyume chake ni kuikosesha mapato Serikali na kuudumaza Wakala kiutendaji.

(b) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kulipa kipaumbele suala la ununuzi wa mitambo mipya na ya kisasa kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kwani fedha hizo zimeidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika bajeti ya mwaka 2021/2022. Kamati haijaridhishwa na kusikitishwa pia na ucheleweshwaji wa kupatiwa fedha hizo Wakala.

(c) Kamati pia inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikali kuharakisha upatikanaji wa kibali cha uajiri wa nafasi sita (6) zilizo wazi kwa Wakala zilizotokana na watendaji wake kuustaafu. Nafasi ambazo mchakato wake ulikuwa umeshakamilika.

(d) Kamati vile vile inaishauri Serikali kufanya mazungumzo na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda pamoja na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maaliasili na Mifugo kuupatia Wakala wa Uchapaji ghala ili kuwasaidia kuhifadhia vifaa vyao vya Bohari na kuondokana na kukodi maghala ya Watu Binafsi na kwa fedha nyingi.

(e) Kamati inawashauri wasambazaji na wazalishaji wetu wa ndani na nje kuunga mkono juhudi za Serikali za matumizi ya mfumo wa Kielektroniki wa manunuzi uliopo kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

## 5.6 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu pamoja na Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo Zanzibar ambapo kupitia Programu hii, huduma mbali mbali hutolewa kama vile Ukaguzi wa Filamu na Sanaa za

Maonesho, Uendelezaji wa Matumizi Sahihi ya Kiswahili, Kusajili na Kusimamia Hakimiliki, Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo Zanzibar, Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa Pamoja na Usimamizi wa Vyama vya Michezo. Jumla ya Tanzania shilingi Bilioni Kumi na Tano, Milioni Nane na Arubaini, Laki Tisa na Sabini na Moja (15,840,971,000/=) zilipangwa kutumika.

**BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR**

Baraza la Michezo la Taifa Zanzibar (BTMZ) limeanzishwa chini ya Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo, Nambari 5 ya mwaka 2010. Miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kusajili na kusimamia vyama vya michezo pamoja na kukuza na kuendeleza michezo katika ngazi zote hapa Zanzibar.
Aidha, Baraza katika utekelezaji wake limefanikiwa kuanzisha mchezo wa ngumi hapa Zanzibar baada ya kuruhusiwa rasmi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baraza limefanikiwa kuunda na kuutangaza uongozi wa muda wa kusimamia, kuendesha mchezo pamoja na kuwekwa kwa taratibu za kuusajili rasmi mchezo huo.

Vile vile, Baraza mnamo mwezi wa Oktoba, 2022 limefanikiwa kukutana katika kikao cha pamoja na viongozi wa BMT na BMTZ ili kujadili na kuzipata ufumbuzi changamoto za mchezo wa netball kwa kujenga mashirikiano mazuri ya vyama hizo.

**CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZANZIBAR**

(a) Uhaba wa fedha unapelekea Baraza la Michezo la Taifa kushindwa kutekeleza kwa ufanisi shughuli walizojipangia kwa mujibu wa Mpango kazi na bajeti husika.

(b) Ukosefu wa usafiri wa kudumu wa ufuatiliaji wa kazi za kila siku za Baraza.

(c) Uhaba wa fedha na wafadhili kwa Vyama vya michezo hali inayopelekea vyama hivyo kutegemea fedha za kuendesha michezo kutoka Baraza la Michezo.

(d) Kupotea na kusahaulika kwa baadhi ya michezo ya jadi Visiwani mwetu.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kupitia Baraza la Michezo la Taifa kuandaa utaratibu wa kukutana na Wazee katika Wilaya zote Unguja na Pemba kwa ajili ya kujadili juu ya suala zima ya kuienzi, kuitunza na kuiendeleza michezo ya jadi iliopo ndani ya Visiwa vyetu ili isije kupotea kabisa katika karne zijazo.

(b) Kamati pia inaupongeza Uongozi wa Wizara kwa kuhakikisha kuwa michezo inaendelezwa Visiwani mwetu pamoja na kukuza vipaji kwa vijana wetu ili waweze kujitegemea na kujiajiri wenyewe bila ya kutegemea ajira kutoka Serikalini.

(c) Kamati inaishauri Serikali kuiongezea bajeti Baraza la Michezo la Taifa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Baraza pamoja uendeshaji wa shughuli za Michezo kwani hivi sasa Baraza limekuwa likishindwa

kutekeleza vyema majukumu yake. Ili kupunguza kutegemea Misaada na wafadhili.

(d) Kamati inaishauri Serikali katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kuitengea fedha kwa ajili ya ununuzi wa gari ya kudumu ya Baraza la Michezo la Taifa ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi.

## 5.7 PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA

Kiujumla utekelezaji wa Programu Kuu hii unajumuisha Programu Ndogo Tatu nazo ni Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Tafiti, Programu Ndogo ya Utumishi na Uendeshaji na Programu Ndogo ya Uratibu wa Wizara Ofisi Kuu Pemba. Fedha iliyotengwa kutumika katika Programu Kuu hii ni jumla ya Tanzania shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Mbili na Kumi na Tano na Thelathini Elfu (3,215,030,000/=).

### 5.7.1 PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA TAFITI

Utekelezaji wa Programu Ndogo hii unatokana na utoaji wa huduma mbali mbali ikiwemo Uratibu wa Sera na Tafiti, Kuratibu, Kuandaa na Kuwasilisha Bajeti na Kuratibu Mipango na Miradi ya Maendeleo. Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilifanya ziara ya ukaguzi wa ukarabati unaoendelea wa Uwanja wa Gombani na kubaini changamoto kadhaa za kiutendaji zilizopelekea kazi hiyo kusuasua.

## UKARABATI WA UWANJA WA GOMBANI (PEMBA)

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kupitia utekelezaji wa Programu ya Uendelezaji wa Viwanja vya Michezo kwa mwaka wa bajeti 2021/2022 ilipanga jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Saba (7,000,000,000/=) kwa ajili ya Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo kwa Unguja na Pemba ambapo miongoni mwa shughuli kuu zilizopangwa kutekelezwa katika programu hii ni Ukarabati na Uboreshaji wa Uwanja wa Gombani (Pemba).
Uwanja wa Gombani ni miongoni mwa Viwanja vitatu vikubwa vya michezo hapa Zanzibar vyenye hadhi ya Kimataifa. Serikali imeridhia kupitia Wizara ya Habari kukarabatiwa kiwanja hiki ikiwa ni muendelezo wa kuvitunza na kuviboresha viwanja hivi ili kuwa na hadhi na muonekano wa kisasa.

Kupitia bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali, Wizara imefanikiwa kufunga mkataba na Salem Construction Ltd. Vs JV OSAJU CO. Ltd ambao ndio waliopewa kazi ya kufanya ukarabati na uboreshaji wa Uwanja wa Gombani kwa Zabuni Nambari SMZ/S01/W/ICB/2021 – 2022/20. Kazi ya Ujenzi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Uwanja wa Gombani Pemba ulipanga kukamilika ndani ya kipindi cha miezi mitano (5) ambayo ilitarajiwa kumalizika tarehe 15 Disemba, 2022.

Kwa mujibu wa Mkataba, Mradi huu umepangiwa kugharimu jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Mbili na Laki Nane (2,800,000,000/=) tu kwa ajili ya Ukarabati na Uboreshaji wa Uwanja wa Gombani, hadi kufika Januari, 2023 Kamati ilipopokea taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa

Mradi huu bado mradi huu utekelezaji wake unasuasua na muda wa mkataba wa mwanzo ushapita hivyo kupelekea mradi kuongezwa muda kwa mara ya pili. Licha ya hivyo, kazi zilizokusudiwa kufanywa zipo katika hatua ya asilimia 41 tu ya utekelezaji wake.

Vile vile, Kamati imegundua kwamba Wizara iliingia makubalianao na Kampuni ya 'Diamond Builder Limited' kuwa ndio Mshauri Elekezi (Consultant) wa kazi ya Ukarabati wa Uwanja kwa malipo ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Moja na Ishirini (120,000,000/=) ambapo hadi sasa hakuna malipo yoyote yaliyofanyika kwa Msimamizi huyo.

**CHANGAMOTO ZA UKARABATI NA UBORESHAJI WA UWANJA WA GOMBANI PEMBA**

(a) Hakukuwa na mchoro wa awali wa Uwanja hali ambayo ilipelekea kazi kuchelewa kuanza kwa Mkandarasi kuanza kuchora upya mchoro wa Gombani.
(b) Usafirishaji wa vifaa kutoka China kwa meli ulichelewa kutokana na tatizo la COVID – 19 pamoja na ucheleweshwaji wa fedha za kununulia vifaa hivyo.
(c) Kutangazwa kwa zabuni ya ujenzi wa mradi bila ya kuwepo kwa mchoro halisi wa Uwanja wa Gombani Pemba uliochorwa awali.
(d) Kutangazwa kwa zabuni bila ya kukubalika taratibu za BOQ za ujenzi wa mradi huo.
(e) Matumizi ya fedha za Ujenzi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Kiwanja cha Gombani kuongezeka maradufu tofauti na bei iliyokubalika awali (variation of work).

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuandaa mpango madhubuti wa uhifadhi wa nyaraka za Serikali ili kuepusha matumizi makubwa ya fedha za Serikali kama ilivyojitokeza kwa kazi ya michoro ya Kiwanja cha Gombani, Pemba.

(b) Kamati inaishauri Serikali kuwa na kikosi kazi cha tathmini ufuatiliaji wa mikataba inayoingia Serikali katika kazi zote za miradi mikubwa. Kwani Kamati imebaini baadhi ya watendaji huibebesha mzigo mkubwa Serikali wakati mkandarasi huyo tayari kapewa muda wa ziada (addendum) zaidi ya mara moja kwa kazi hiyo.

(c) Pia, Kamati inaishauri Serikali kuwepo kwa mafunzo maalum kwa watendaji wetu wanaohusika moja kwa moja na usimamizi wa miradi ya Serikali ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali kwani Kamati imegundua katika mradi wa Ujenzi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Uwanja wa Mchezo Gombani kuwa umekiuka baadhi ya taratibu za kisheria za utoaji wa tenda ya Zabuni ya ujenzi huu ambapo zabuni imetangazwa bila ya kuwepo kwa mchoro na hata hiyo BOQ iliotolewa kwa ajili ya wakandarasi kuomba kazi ilikuwa haijakamilika.

## 5.7.2 PROGRAMU NDOGO YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Dhumuni kuu la kuanzishwa kwa Programu Ndogo hii ni kutoa huduma ya kuwajengea uwezo na mazingira mazuri ya kwa wafanyakazi pamoja

na usimamizi wa Mpango wa Manunuzi na Matumizi ya Fedha kwa Wizara.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**

(a) Kucheleweshwa kuingizwa fedha za miradi ya Wizara kwa wakati ambapo Wizara imeshakamilisha hatua zote za kufunga mikataba na wazabuni kwa miradi minne ikiwemo:
   (i) Programu ya Urushaji wa Matangazo ya ZBC,
   (ii) Pia imekamilisha hatua zote za ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapaji,
   (iii) Malipo ya Mshauri Elekezi kwa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Ushoni na Mabanda ya Kuku,
   (iv) Ukarabati wa Uwanja wa Gombani;
(b) Wizara kuingiziwa fedha za matumizi mengineyo (OC) chache tofauti na matumizi halisi ambalo linakwamisha utekelezaji wa baadhi ya shughuli zilizopangwa kwa mwaka wa bajeti husika.
(c) Ugumu wa kufanya malipo ya mirabaha kwa watumiaji wa kazi za Hakimiliki kibiashara, wakiwemo wawekezaji wazawa, baadhi ya mahoteli, vituo vya utangazaji vya binafsi, vyombo vya usafiri wa majini, watumiaji wa kazi za maandishi kama vile Taasisi za Elimu ya Juu, Skuli za Binafsi na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
(d) Kuwepo kwa changamoto ya uharamia wa Hakimiliki ambapo kazi za Sheria jambo ambalo linakosesha wasanii haki zao.
(e) Vyama vya Michezo kutegemea kwa asilimia mia moja (100) ruzuku kutoka Serikalini katika kuendesha shughuli zao.

(f) Uhaba wa viwanja vya michezo vya ndani na nje kama vile mpira wa ukuta, mpira wa vinyoya, 'Golf', 'Hocky' na 'Criket' jambo ambalo linapelekea kupunguza ushiriki wa michezo hiyo kutokana na kukosekana kwa maeneo ya kufanyia mazoezi na mashindano ya michezo hiyo.

(g) Kuwepo kwa ongezeko kubwa la kazi za ziada nje ya 'BOQ' ya awali kwa Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani kunakopelekea ongezeko la kazi za ziada (variations).

(h) Kutokuwepo kwa uhifadhi mzuri wa nyaraka za Serikali ambapo Kamati imebaini kutokuwepo kwa michoro kwa viwanja vyote vya vilivyojengwa Zanzibar ikiwemo uwanja wa Gombani, Amani na Mao-Tse-Tung.

(i) Kutokamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya vitano (5) ambavyo ni Kishindeni, Kangani, Mkokotoni, Kitogani na Kama, ambapo vimechukuwa muda mrefu tokea awamu ya saba hadi leo mradi huo umekuwa wa kusuasua.

(j) Kutokuwa na jengo la kudumu la Ofisi ya Tume ya Utangazaji ambapo inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kukodi jengo la binafsi kwa matumizi ya ofisi takribani Tanzania Shilingi Milioni Thelathini na Tatu na Laki Moja na Ishirini (33,120,000/=) kwa mwaka.

(k) Upatikanaji mdogo wa fedha za Miradi ya Maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ilipangiwa kupatiwa Tanzania Shilingi Bilioni Thelathini Mbili (32,000,000,000/=) hadi kufikia Disemba, 2022 fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji ni asilimia 2 tu.

(l) Kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, Shirika la Magazeti ya Serikali

pamoja na Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi Binafsi yanayotokana na huduma mbali mbali kama vile uchapaji, utangazaji wa matangazo, urushaji wa vipindi, usambazaji wa magazeti kwa Serikali na Taasisi Binafsi n.k.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaishauri Serikali kuipatia fedha za Miradi ya Maendeleo Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili iweze kutekeleza na kukamilisha miradi hiyo kwa wakati kama fedha zilivyoidhinishwa kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023. Fedha iliyopangwa ilikuwa ni Tanzania Shilingi Milioni Ishirini Tatu, Laki Nane na Ishirini na Tisa (23,829,000.00/= hadi kufikia Disemba fedha iliyopatikana ni Tanzania Shilingi Milioni Mia Tano na Sitini (560,000,000/=) sawa asilimia 2.4.

(b) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuliangalia kwa kina suala la ongezeko la matumizi ya ziada katika Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani (variations) ambapo ongezeko hilo Kamati imegundua limetokana na kutokuwepo kwa michoro ya awali ya uwanja huo na wakandarasi kuomba kwa BOQ ambapo haikukamilika iliyotolewa na Wizara.

(c) Kamati inapendekeza kwa Serikali kusimamia uamuzi uliotolewa na Baraza la Mapinduzi juu ya suala zima la kulipwa kwa madeni wanayodai kwa baadhi ya Taasisi za Serikali na Binafsi ili Taasisi hizo ziweze kujiendesha wenyewe bila ya kutegemea fedha kutoka Serikali.

(d) Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiongezea fedha ya matumizi mengineyo (OC) Wizara ya

Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2022 ilikadiriwa kupatiwa Tanzania Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja na Sabini na Tisa (2,179,000,000/=) na fedha zilizopatikana ni Tanzania Shilingi Milioni Mia Saba Hamsini na Nane, Laki Mbili na Tisini na Nne (758,294,000/=) kwa matumizi ya Wizara pamoja na Taasisi zake sawa na asilimia 35.

(e) Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuandaa mpango wa kujenga viwanja vya michezo ya ndani kwa kushirikiana na Wahisani/Wadau ama Wafadhili ili kuweza kuwa na viwanja vingi vya michezo hiyo kwa lengo la kutoa fursa zaidi kwa vijana wenye vipaji katika michezo hiyo ambapo ni moja ya sehemu ya ajira kwao.

(f) Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwapatia eneo la kujenga ofisi ya kudumu Tume ya Utangazaji Zanzibar ili kuondokana na malipo makubwa ya kodi ya majengo binafsi.

(g) Kamati inaishauri Serikali kuwaingizia fedha Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa ajili ya kufanya malipo ya deni wanalodaiwa Shirika la Utangazaji la Zanzibar kwa vifaa walivyoviagiza vya “Live U” vyenye gharama jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Tano (500,000,000/=).

(h) Kamati inapendekeza kwa Serikali kuwepo kwa mfumo maalum wa uhifadhi wa nyaraka na uwekaji wa kumbukumbu za Serikali kwani Kamati imebaini kukosekana kwa baadhi ya nyaraka hizo kunapelekea kuigharimu Serikali kufanya matumizi nje ya mpango wa bajeti kwa mwaka na mradi husika.

(i) Kamati inaishauri Wizara kuzifanyia marekebisho Sheria zote ambazo zina mapungufu ili kuleta ufanisi na tija kwenye utekelezaji wa kazi za Wizara,

(j) Kamati inaipongeza Wizara kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa uzalendo mkubwa na ubunifu licha ya uhaba wa rasilimali watu na fedha.

## SEHEMU YA TATU

## 6. HITIMISHO

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote kwa ujumla wa Wizara zote Nne zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi zote pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati inapokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Kamati inampongeza kwa dhati kabisa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati Ndg. Khamis Hamadi Haji pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti yake kwa mwaka 2022/2023. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.

Mwisho kabisa na kwa umuhimu mkubwa Kamati inawapongeza kwa dhati kabisa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa

Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2025.